# Mungu Aliye Mwingi Wa Rehema

Phoenix, Arizona, USA
Januari 19, 1965

1 Mnaweza kuketi. Nilikuwa … ama kubeba, kuja na kumwona Ndugu Moore na hao wote hapa jukwaani, marafiki ambao nimewajua kwa miaka mingi sana. Hakika ni majaliwa kuwaona hapa usiku wa leo. Ninajisikia mdogo kusimama hapa na kuzungumza na wanatheolojia kama hawa nyuma yangu, na labda watanisahihisha ninapokosea. Natumaini hivyo.

Tuna furaha sana usiku wa leo kuwa na mtu fulani hapa, Dada Rose. Tulikuwa tunashuka kuja … Nilikuwa pamoja na Ndugu Shores na msaidizi wake, leo, kwa chakula kidogo cha mchana. Na tukienda barabarani, Ndugu Williams alisema ya kwamba Dada Rose alikuwa mgonjwa sana. Nasi tukaingia kumwona kwa muda kidogo tu, tukapiga magoti. Naye alikuwa na homa kali, na ni mgonjwa sana. Maneno machache tu ya maombi, na Bwana akanena nasi, na kusema, "Ataponywa." Kasema, "Atakuwapo kesho usiku," wanasema. Naye yuko hapa usiku wa leo, ameketi papa hapa. Hiyo ni kweli.

2 Dada Rose, simama kidogo, ili kwamba wao … Tunamshukuru Bwana. Alikuwa amelala kitandani. Akasema, "I—ibilisi alinipiga tu kutoka kwa kila kitu. Nilikuja hapa na kuugua ugonjwa huu," namna fulani ya ugonjwa wa koo, na kadhalika. Lakini Bwana amemaliza, kwa hiyo tuna furaha. Tukimshukuru Bwana mpendwa!

Sasa tumekuwa na nyakati nzuri sana. Na kesho usiku, sasa, tunaenda kule—kule Ramada. Na msisahau sasa, haitakuwa hapa kesho usiku, itakuwa ni huko Ramada. Na mkutano utaanza usiku unaofuata. Inanibidi kunivumilia usiku mmoja zaidi, unajua.

3 Kwa hivyo usiku wa jana nili—nilipita kipimo sana, nami nikajiahidia kidogo ya kwamba tangu mwanzoni mwa mwaka kwamba nitazifupisha jumbe hizi kutoka masaa matatu ama manne, masaa matano, hata labda dakika thelathini ama arobaini. Na kama nilivyowaambia jana usiku, mke wangu alitoa maoni yangu Jumapili, akasema, "Ulifanya vizuri sana." Kwa—kwa hiyo basi, hakika ikanibidi kuja huku jana usiku na nikaharibu, mnaona, kuhusu muda. Lakini nilikuwa na dakika hamsini na tano, badala ya thelathini, jana usiku.

Akishuka, usiku wa leo, Billy akasema, "Utazungumzia nini?"

Nikasema, "Vema, nina maandishi machache yaliyoandikwa hapa, na Maandiko machache. Sijui, baadhi ya mengine, jumbe nne au tano tofauti." Nikasema, "Ninajisikia ninapofika kule chini, na kuona kile kinachoendelea."

Kasema, "Uliahidi kuwaombea hao wagonjwa wote."

Nikasema, "Naam, bwana. Una kadi ngapi?"

Kasema, "mia mbili."

Nikasema, "Afadhali nianzie, usiku wa leo."

Naye akasema, "Sasa kumbuka, unapata tu dakika kumi na tano za kuzungumza." Kasema, "Ulichukua zilizosalia jana usiku." [Ndugu Branham na kusanyiko wanacheka — Mh.] Itatubidi kuharakisha, sivyo?

4 Vema, tulifanya ahadi kwenu, ya kwamba tutawaombea hao watu waliokuwa na kadi za maombi, nasi tuna—tunawajibika kwa ahadi, bila shaka. Hatuwezi kuwaleta wote kwenye mistari hii, wala wala nisingeweza kuwaita mmoja mmoja, huko kwenye wasikilizaji. Hata ingawa Roho Mtakatifu angenionyesha, si-sitaweza kufanya hivyo. Najisikia uzito ndani yangu. Na, lakini sote tunafahamu mambo hayo. Tunajua ya kwamba Mungu angali ni Mungu. Siyo kwamba hayo ndiyo yanayoponya. Ni kwamba hilo tu linajenga imani, kutufanya tujue ya kwamba—ya kwamba tuko katika Uwepo Wake.

Nasi tunaenda, usiku wa leo, kuwaombea hao wagonjwa wote, kila mmoja wao aliye na hizo kadi za maombi, apate kuombewa. Na halafu kesho usiku, kule Ramada, tutajaribu kutoa mengine na tuanze kuwaombea kule, maana ningali nina kesho usiku. Nami nafikiri nina usiku mmoja wa mkutano, labda kiamshakinywa pia. Inategemea jinsi mambo yanavyotokea.

5 Kuna wengine, mmoja wa wahubiri ambaye hakuweza kufika; na hata sasa bado hajafika; sidhani. Ndugu Humburg, ama hiyo ni … [Ndugu fulani anasema, "Amburgy." - Mh.] Amburgy, Amburgy, Kash Amburgy. Kwa hiyo ni—ninakosea kabisa, hilo ni jina la Kijerumani. Na—nadhani hicho ni Kijerumani. Kwa hiyo huenda inanipasa kwa namna fulani kugugumiza jina, kama tunavyosema, samahani kwa tamshi hilo, kwake.

Kwa hiyo tumekuwa na wakati mzuri sana katika Bwana, hata hivyo. Kwenu nyote, kama kuna wageni hapa usiku wa leo, hakika tuna furaha kuwa pamoja nanyi, na tunatumaini ya kwamba Bwana atawabariki. Ninaomba ya kwamba hakutakuwako na wagonjwa wowote jengoni tutakapoondoka usiku wa leo, kwamba Bwana wetu atashuka katika nguvu Zake kuu na atawaponya wote walio wagonjwa na

wanaoteseka.

6 Hapa wakati fulani uliopita, nilikuwa nikiwachukua watu binafsi kwenye mahojiano maalum, baadhi ya mambo magumu ambayo hatungeweza kuyamaliza. Ndipo watu waliongezeka sana, hata ikawa Bwana alizidi kutubariki, hata tukafikia kuwa na watu mia tatu au mia nne waliokuwa wakingojea kuingia kwa zamu, kwa hiyo watu wengine waliudhika kwa sababu iliwabidi kusubiri. Labda katika muda huo ingekupasa usubiri labda mwaka mmoja au miwili ili upate nafasi ya kuingia, mnaona, katika nafasi kati ya mkutano mmoja na mwingine ili kuwa na mahojiano ya kibinafsi. Nasi tungeketi tu na kumngojea Bwana mpaka Yeye atuambie kisa hasa.

Hakuna shaka kuna watu wanaoketi hapa usiku wa leo ambao wamekuwa kwenye mahojiano hayo maalum. Wapo? Hebu tuone mkiinua mikono yenu. Kwenye mahojiano maalum. Naam, hao hapo, kwa hiyo, na mnajua hiyo ni kweli. Tunangojea tu kuona yale Bwana angesema, jinsi kesi hiyo … Na basi ilinibidi kukomesha jambo hilo hapa wakati fulani uliopita. Nilimwambia Billy ya kwamba tusingeweza kuwa na mahojiano mengine ya kibinafsi.

7 Mwaona, ni—-ni—nimepita tu umri wa miaka ishirini na mitano mara ya pili hivi karibuni, na ninakaribia mara ya tatu. Na kwa hiyo unapozeeka kidogo, mbona, huna, wewe … kwa namna fulani huwezi kuendelea kama ulivyokuwa ukifanya. Hatua zako zinakuwa fupika. Na—na, bila shaka, Ndugu Moore bado hajui lolote kuhusu hilo. Yeye … Nafikiri tuko mahali fulani karibu na umri ule ule.

Bali maji mengi yametiririka mtoni tangu mimi na wewe, na ndugu Brown tulipokuja hapa mara ya kwanza, pamoja na ndugu Outlaw na ndugu Garcia, na ndugu Fuller. Sijui kama hao watu wangekuwa humu usiku wa leo? Ndugu Garcia, Ndugu Fuller, Ndugu Outlaw, wako hapa? Inueni mikono yenu kama mpo. Naam, yupo Ndugu Fuller, ninaamini, kama sijakosea. Ndugu Outlaw hapa. Ndugu Garcia, na—naamini ingawa aliondoka Phoenix. Nafikiri hiyo ni kweli. Yeye—yeye aliondoka Phoenix, naye yuko huko California. Vema, bila shaka zilikuwa siku zenye fahari, nami ningali nauamini ujumbe ule ule niliokuwa nao wakati huo, "Yesu Kristo, Yeye yule jana, leo na hata milele. Nadhani hiyo imekuwa kama … Vema, Becky alikuwa mtoto mchanga. Hiyo ni kama miaka kumi na tisa.

Na sasa yeye ni mkubwa, amekua, mnene, mwenye sura mbaya akiketi mahali fulani pale, umri wa miaka kumi na tisa. Uko wapi, Becky? Jamani, nitajuta kwa kusema hayo. Ninakumbuka nilimbeba mkononi mwangu. Hakika ningekuwa na kazi ya kufanya jambo hilo usiku wa leo.

8 Kumbukeni kule kwenye kanisa la Ndugu Garcia usiku mmoja, yeye alikuwa jamaa mdogo sana. Nami nikasema, "Tuna mkutano wa kimataifa usiku wa leo." Nikasema, "Ninazungumza na Wahispania." Nami nikasema, "Mke wangu hapa ni Mjerumani." Nikasema, "Mimi ni Mu-Airishi." Nami nikasema, "Na msichana wangu mdogo ni Mhindi," na huyo alikuwa Becky.

Kwa hiyo wakati nilipotoka kwenye mlango wa nyuma, kulikuwa na msichana mdogo wa Kimeksiko huko nje, kasema, "Ndugu Branham!"

Kasema, "Naam, mpenzi, unataka nini?"

Akasema, "Je hudhani mtoto wako ni mweupe kidogo, hawezi kuwa Mhindi?" Yeye ni rangi ya dhahabu, mwajua.

Nami nikasema, "Ni Mhindi kwa tabia."

Basi tunashukuru kwa kuwa hapa tena usiku huu. Sasa kabla hatujaliendea Neno, hebu tumkaribie, kwa kuwa Yeye ni Neno. Wakati Neno linapodhihirishwa, huyo ni Yeye ndani yako.

9 Kama tulivyohubiri jana usiku juu ya *Mbegu Yenye Hitilafu*, mlipendezwa na hizo, baraka za Bwana? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Ni—kwa kweli nilifurahia kuwaletea Ujumbe. Nasi tunaona jinsi mbegu zilivyo.

Sasa kuna haja maalum usiku wa leo, kitu fulani maalum tu? Labda baadhi yenu ninyi nyote ambao mtakuwa kwenye mstari huu wa maombi, mseme, "Mungu, turehemu. Ninapokuja kuombewa, imani yangu na iinuke ipate kutimiza masharti hayo." Na—na labda mtu fulani ana mpendwa, mgonjwa, na kitu fulani. Ungeweza tu kuinua mkono wako ili Mungu aangalie tu chini na kusema … Sasa kama hiyo … Hujui jinsi hilo linanifanya nijisikie kuangalia kule. Angalia tu haja ndani hapa! Ndugu wahudumu, angalieni tu jambo hilo. Mnaona? Sasa, kama inanifanya nijisikie hivyo, inamfanya nini Baba yetu? Hakika.

Sasa hebu tuombe.

10 Mpendwa Yesu, tunakaribia sasa kile Kiti cha Enzi cha rehema, kupitia Jina hili linalojitosheleza kabisa. "Kwa maana hapana jina jingine walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo, bali hili Jina la Bwana Yesu pekee". Nasi tunakuja katika Jina Lake. Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba utatupokea, usiku wa leo, kama watoto Wako wanaoamini. Na utusamehe kutokuamini kwetu, Bwana. Tusaidie usiku wa leo, huenda ikawa kwamba tutaamini kabisa kila Neno la Mungu usiku wa leo,

kwa ajili ya mambo yote tunayohitaji.

Unajua yote yaliyo chini ya mikono hii iliyoinuliwa; kuna magonjwa, labda wengine wao ni shida za kinyumbani, wengine wao ni shida za kifedha, wengine wao uchovu, labda wengine walianguka, wengine ni wenye dhambi. Hata iwe shida gani, Wewe u zaidi ya adui yeyote. Kwa hiyo tunaomba, Bwana, ya kwamba—ya kwamba usiku wa leo, ya kwamba tutatambua ya kwamba adui zetu, kila mmoja, ameshindwa, hata mauti yenyewe. Na kwamba sisi ni zaidi ya washindi katika Yeye Ambaye—Ambaye alitupenda na kujitoa Mwenyewe kwa ajili yetu, ametuosha katika Damu Yake.

11 Tunaomba, Bwana, kwamba kutokuamini kote, mashaka yote, mapingamizi yote, na yale yote yasiyofanana na Mungu yatukimbie usiku huu, ili Roho Mtakatifu apate mamlaka mioyoni mwetu. Jalia azungumze nasi katika njia za kisiri. Jalia azungumze nasi katika Nguvu Zake. Jalia awafufue wale walio—waliokufa kiroho, awarudishie afya wale walio wagonjwa na wanaoteseka, ainue magoti yaliyo dhaifu, mikono iliyochoka ambayo inaning'inia chini. Na jalia kuwe na wakati wa kufurahi.

Na ianze usiku huu, Bwana, tuondoke hapa kwenda Hoteli ya Ramada na kuanzisha mmoja kati ya mikutano mikuu sana iliyowahi kuwako katika mji huu. Bwana, tunapokusanyika pamoja na kuomba! Ulisema, "Ikiwa watu walioitwa kwa Jina Langu, watajikusanya wenyewe pamoja na kuomba, ndipo Nitasikia kutoka Mbinguni." Mungu, tunaomba ya kwamba jambo hili litakuwa hivyo, usiku wa leo.

Sasa, Baba, tunapolisoma Neno, hakuna mtu anayeweza kulifasiri ila Wewe, Wewe ndiwe mfasiri Wako Mwenyewe, nasi tunaomba ya kwamba utatufasiria mambo tunayosoma usiku wa leo. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

12 Sasa kama wengi wenu mnataka kuandika Maandiko ambayo mhudumu anasoma. Nami ningetaka ninyi, usiku wa leo, kama mkipenda, mfungue Waefeso.

Nami nilikuwa nikizungumza Jumapili iliyopita juu ya Waefeso, jinsi ambavyo Kitabu cha Yoshua kilikuwa Waefeso wa Agano la Kale, na jinsi kilivyokuwa Kitabu cha ukombozi.

Na ukombozi una sehemu mbili tofauti, "Kutoka nje ya" na "Kuingia ndani ya." Kwanza, huna budi kutoka. Watu wengine wanataka kuingia pamoja na ulimwengu; bali huna budi kutoka ulimwenguni, kuingia katika Kristo. Huna budi kutoka katika kutokuamini, kuingia katika imani. Hakuwezi kuwa na kitu kimoja njiani mwako. Ili kweli uwe na imani halisi, huna budi kuacha kila kitu kilicho kinyume na Neno la Mungu, nyuma, kuingia katika imani.

Na hicho kilikuwa ni Kitabu cha Waefeso wa Agano la Kale, Yoshua. Ambapo, Musa aliwakilisha torati, asingeweza kumwokoa mtu ye yote; bali neema ingeweza, na hapa Yoshua ni neno lile lile kama Yesu, "Yehova-mwokozi."

Na sasa basi, tunaona ya kwamba tumekuja kwa Waefeso nyingine, Efeso nyingine sasa. Ambapo basi katika madhehebu yetu ya kiakili na mengineyo, na mipango yetu yote ya elimu, imekuja kwenye Yordani ya—yake, ndipo inatupasa kuwa na—na Waefeso tena. Hatuna budi kuwa na kutoka, "kutoka" na "kuingia," kwa ajili ya Kunyakuliwa.

13 Sasa tutasoma usiku wa leo kutoka sura ya 2 ya Waefeso. Nilikuwa nikisema hayo tu ili mfungue ma—mahali hapo, ama mfungue hiyo sura.

> *Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu;*
>
> *Ambazo mliziendea zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu, na kwa kumfuata mfalme wa uwezo wa anga, roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi;*
>
> *Ambao zamani, sisi sote nasi tulienenda kati yao, katika tamaa za miili yetu, tulipoyatimiza mapenzi ya mwili na ya nia, tukawa kwa tabia yetu watoto wa hasira kama na hao wengine.*
>
> *Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda;*
>
> *Hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo; yaani, tumeokolewa kwa neema.*

Ninataka kuchukua kutoka hapo machache, ama sehemu ya kifungu hiki, "bali Mungu," *Mungu aliye mwingi wa rehema.*

14 Nataka ninyi mwone hapa ambavyo nabii, mtume, namaanisha Paulo, ambaye—ambaye, alivyotaja hili, ambavyo, "Ninyi amewahuisha mliokuwa wafu. Ninyi amewahuisha ambao hapo kwanza mlikuwa wafu, wafu katika dhambi na makosa; mkifuata mambo ya ulimwengu, mapenzi ya mwili, na mkitimiza mapenzi ya nia. Ana …"

Ni kitu gani kilichosababisha badiliko hili, mnaona? Ni nini kilichosababisha hayo, "kutoka wakati

mlipokuwa wafu", hata kuhuishwa? *Kuhuisha* maana yake ni "kufanywa hai." Kulikuwako na badiliko, kutoka mautini kuingia Uzimani. Hakuna mwingine, hakuna jambo lingine ambalo lingeweza kumpata mtu ye yote, mkuu sana, hata kumbadilisha kutoka mautini kuingia Uzimani. Mtu, kama alikuwa akifa, kimwili, na angeweza kuponywa kimwili, hilo lingekuwa ni jambo kuu, bali hakuna kitu kikubwa sana kama wakati amekufa kiroho na Mungu amemhuisha kwa Uzima.

15 "Ninyi zamani, katika nyakati zilizopita, mmekufa." Ulikuwa umekufa. Hata wengi hapa usiku huu, wakati mmoja mnaweza kutazama nyuma na kuona kuwa mlikuwa wafu. Bali sasa mbona ninyi si wafu usiku huu, kama mlivyokuwa wakati huo? Unastahili kuwa hivyo, kwa sababu ulikuwa mwenye dhambi, "bali Mungu aliye mwingi wa rehema." Hilo ndilo—hilo ndilo jambo lenyewe, "Mungu Ambaye alikuwa tajiri." Mambo haya yote tuliyokuwa, "bali Mungu"! Hilo lilifanya badiliko papo hapo, "Mungu aliye mwingi wa rehema"!

Loo, nina furaha sana kwa ajili ya jambo hilo, ya kwamba Yeye ni mwingi wa rehema. Kama angalikuwa tu tajiri wa pesa, kama alikuwa tu tajiri wa vifaa, na hivyo ndivyo alivyo, lakini hata hivyo jambo kuu sana ni kuwa mwingi wa rehema. Loo, hilo ni neno kuu jinsi gani, jinsi ambavyo wakati mmoja tulikuwa tumekufa.

16 Nasi tulikuwa tukizungumza usiku wa juzijuzi juu ya jinsi ambavyo mbegu haina budi kufa. Na kila kitu karibu na chembechembe hiyo ya uhai haipaswi kufa tu, bali kuoza. Kama haiozi, haiwezi kuishi. Na kuoza ni, "kuharibiwa kabisa; imekwisha." Na hata tutakapofikia mahali ambapo maoni yetu na mawazo yetu yamekwisha kabisa na kuoza kabisa kutoka ndani yetu, ndipo chembechembe ya uhai itaweza kuanza kuishi.

Sasa—sasa huenda tukaweza, huenda nikaingiza mafundisho machache tu hapa, ili nisije … Kama huamini, vema. Hilo ni sawa tu. Ninaamini jambo hilo. Naamini ya kwamba—kwamba binadamu anapozaliwa katika ulimwengu huu, anapokuwa mtoto mchanga, aliyezaliwa ulimwenguni, hungeweza kuwa hapa bila ya Mungu kujua tangu milele, kwa sababu Yeye hana mwisho, Yeye anajua mambo yote. Na wakati mtoto huyo mchanga anapozaliwa ulimwenguni, kuna kitu fulani katika mtoto huyo. Kama atapata Uzima, kuna kitu fulani kidogo mle ndani, ndani ya mtoto huyo basi, ambacho yeye atakifikia, mapema ama baadaye. Mbegu hiyo ndogo iko ndani yake. Sasa kama utachukua … Maandiko yanatangaza jambo hilo dhahiri.

17 Sasa kama una Uzima wa Milele usiku wa leo, kama tuna Uzima wa Milele, basi daima tulikuwako, kwa sababu kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele. Daima tulikuwa hivyo. Na sababu ya sisi kuwa, kwa sababu sisi ni sehemu ya Mungu. Na Mungu ndiye kitu pekee kilicho cha Milele.

Na kama Melkizedeki alivyopokea sehemu ya kumi kutoka kwa Ibrahimu, na ilitolewa kwa mjukuu wake, Lawi, ambaye alikuwa bado katika viuno vya Ibrahimu; alitoa fungu la kumi, kwa maana alikuwa bado katika viuno vya Ibrahimu wakati alipokutana na Melkizedeki. Ninataka kuzungumza juu ya jambo hilo kule mahali pengine, asubuhi moja. *Huyu Melkizedeki Ni Nani?* Sasa angalia jambo hilo. Huko nyuma kabisa, Mungu alimjua mvulana huyu akishuka. Yeye alijua mambo yote.

Sasa sisi ni sehemu ya Mungu. Ulikuwa hivyo daima. Hukumbuki jambo hilo, kwa sababu ulikuwa tu sifa katika Mungu. Ulikuwa tu katika mawazo Yake. Jina lako lenyewe, kama liliwahi kuwa kwenye Kitabu cha Uzima, liliwekwa pale kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Yeye alijua ulivyokuwa.

18 Ninasema tu hili, si kuchanganya mafundisho, bali kulinyosha, ili kwamba tuondoke kwenye woga huu na hofu. Hujui wewe ni nani. Hamtakuwa, bali sasa ninyi ni wana wa Mungu. Mnaona, sikuzote mlikuwa wana wa Mungu. Mnaona?

Kwa maana wakati Mungu alipokuweka katika mawazo Yake hapo mwanzo, huna budi kuwa, sehemu fulani yako, Uhai wako ulio ndani yako sasa, ulipaswa kuwa pamoja na Mungu kabla ya hapo. Vema, wakati Yeye, kabla Yeye hata hajafanyika wa kimwili hapa duniani, kabla hakujakuwako na cho chote, bali Mungu, ulikuwa mmoja wa sifa Zake. Yeye alijua jina lako lingekuwa nani. Yeye alijua rangi ya nywele ambayo ungekuwa nayo. Yeye alijua yote kukuhusu. Jambo pekee lililotukia ni wakati wewe, ukiwa mwenye dhambi …

19 Wengi wenu mna—mnaweza kushiriki pamoja nami juu ya wazo hili. Wakati ulipokuwa mvulana mdogo, ama msichana mdogo, ungetembea huku na huko na kungekuwa na mambo fulani ambayo yangekuwa tu, ambapo hayangewasumbua watoto wengine, ilionekana kana kwamba kulikuwa na kitu fulani ndani yako kilicholia. Kulikuwa na Mungu mahali fulani, hata hivyo ulikuwa mwenye dhambi. Mnakumbuka jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Hakika. Sasa hiyo ilikuwa ni nini? Huo ulikuwa ndio huo Uhai mdogo ndani yako wakati huo.

Na halafu baada ya kitambo kidogo, mkaisikia Injili. Labda uliienda kanisani, ukachagua *hiki* na *kile*, kisha ukaondoka kutoka kwenye dhehebu moja hadi jingine. Lakini siku moja, wewe ukiwa sehemu ya Mungu, ilibidi uwe sehemu ya Neno. Na wakati uliposikia Neno, unajua mahali ulikotoka, ulijua Kweli ilikuwa

ni nini. Ulikuwa daima, mbegu ilikuwa ndani yako daima. Neno liliona Neno lililokuwa ndani yako, lililokuwako kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, liliona Neno nawe ukaja Kwake.

20 Kama vile hadithi yangu ndogo ya tai, ya jinsi yule tai mdogo alivyoanguliwa chini ya kuku. Ndipo maskini jamaa huyo akatembea pamoja na hao kuku, yeye, yule kuku akalia, naye hakuelewa mlio wake. Na—na hao kuku wadogo, chakula chao walichokuwa nacho kwenye kitalu, yeye—yeye hakufahamu jambo hilo, jinsi walivyofanya jambo hilo. Lakini kulikuwa na kitu fulani ndani yake, kilionekana kuwa tofauti na vile kuku huyo alivyokuwa, kwa sababu hapo mwanzo alikuwa tai. Hiyo ni kweli. Siku moja mama yake alikuja akimwinda, na, wakati aliposikia mlio huo wa tai, ulikuwa tofauti na mlio wa kuku.

Na hivyo ndivyo ilivyo kwa kila mwamini aliyezaliwa mara ya pili. Unaweza kusikia theolojia yote unayotaka, na hitilafu yote ya kujibunia; bali wakati Neno hilo linapomulika huko nje, basi kuna kitu fulani kinachoshilia, unakuja Kwake. "Ninyi mliokuwa mmekufa katika dhambi (huo uhai) amewahuisha." Lazima kuwe na Uhai pale wa kuhuisha, kwanza. Mungu, kwa kujua Kwake tangu asili, alijua mambo yote. Nasi tulichaguliwa tangu zamani kuwa wana na binti za Mungu. "Ninyi mlipokuwa mmekufa katika dhambi na makosa, ambayo katika sisi sote tulikuwa tumepita nyakati zetu, bali Yeye ametuhuisha."

21 Mwangalie Paulo, wakati Paulo alipokuwa mwanatheolojia mashuhuri. Lakini alipokuja uso kwa uso na Neno hilo, Yesu, lilihuisha. Akawa hai upesi sana, kwa sababu yeye aliamriwa kuwa hivyo. Ninii … Yeye alikuwa sehemu ya Neno; na wakati Neno lilipoliona Neno, ilikuwa ni tabia yake. Mlio wote wa kuku, katika makanisa halisi, haukuwa na matokeo kwake; alikuwa ameliona Neno. Lilikuwa ni sehemu yake. Alikuwa ni tai. Yeye hakuwa kuku; alikuwa tu kwenye kitalu pamoja nao. Lakini yeye alikuwa ni tai, kwanza.

22 Nilisikia hadithi ndogo kama hiyo, natumaini haisikiki ni ya kukufuru, kuhusu bata mdogo kuzaliwa chini ya kuku, wakati mmoja. Asingeweza kuelewa. Maskini jamaa mdogo wa kuchekesha, wa kipekee, naye asingeweza kufahamu mavumbi na kila kitu. Walikuwa wakicheza kwenye kitalu. Lakini siku moja yule mzee kuku aliongoza vifaranga wadogo nyuma ya zizi, naye akapata harufu ya maji. Vema, alitoka akaenda kwenye maji hayo kwa nguvu awezavyo kwenda. Kwa nini? Hakuwa amewahi kuwa kwenye kidimbwi hapo kabla. Hakuwa amewahi kuingia majini. Bali yeye alikuwa ni bata, kwanza. Jambo pekee alilopaswa kufanya lilikuwa ni kujitambua.

Hivyo ndivyo alivyo mwamini. Kuna kitu fulani ndani yake, ambacho, anapokutana na Mungu uso kwa uso, yeye hujitambua. Mbegu hiyo iko ndani yake, na imehuishwa. Jamani, hiyo ni kweli, naye anaruka mbali na mambo ya ulimwengu. Yanakufa kwake. Jamani, ninakumbuka, sote tulikuwa na maisha yetu, katika siku za nyuma, katika mambo hayo ya ulimwengu. Lakini mara tu tuliposhika Kitu hicho halisi, kitu fulani kilichotuhuisha, mbegu ndogo iliyopata Uhai, ndipo mambo yote ya ulimwengu yakaoza papo hapo. Hatukuwa na shauku tena ya jambo hilo.

23 "Yeye aliyezaliwa na Mungu, hatendi dhambi. Mwabudu akiisha kusafishwa mara moja hana tena dhamiri ya dhambi, hana hamu tena ya kutenda dhambi." Swali la dhambi limekwisha. Unakuwa sehemu ya Mungu, katika Kristo. Kristo alikufa apate kukukomboa.

Sasa hebu wazia tu yale yote tungalikuwa kama si Mungu. Lakini Mungu, katika wingi wa rehema Zake, jinsi alivyotukomboa usiku wa leo! Tungekuwa wapi usiku wa leo kama isingekuwa ni kwa wingi wa rehema za Mungu juu yetu?

Wakati mmoja ulimwengu ulikuwa wenye dhambi sana, mwanadamu alikuwa ameuharibu hata Mungu akaghairi kuwa alimuumba mwanadamu. Kichwa chote kilikuwa donda lililooza na kunuka, mwili mzima, Mungu alijutia kumuumba mtu. Kwa hiyo akasema, "Nitamwangamiza mtu niliyemuumba." Atawaangamiza kwa sababu yeye hana kitu ila kundi tu la upotovu.

Na jamii yote ya wanadamu ingeangamizwa wakati huo, lakini Mungu, mwingi wa rehema, asingewaacha wasio na hatia waangamie pamoja na wenye hatia. Naye akaenda na kuwafanyia njia wale waliotaka kuingia, waliotaka kufanya yaliyo mema. Yeye, alifanya njia ya rehema kwa wale waliotaka rehema, Naye akaandaa safina. Kwa maneno mengine, Yeye aliwatia tai Wake mabawa, ili wasizame pamoja na kuku. Lakini Yeye—Yeye alifanya njia ya kutokea, katika siku za Nuhu. Hili lilimfanya Yeye kufanya jambo hilo, kulitimiza, kwa sababu Yeye alikuwa mwingi wa rehema.

24 Lakini baada ya Yeye kuwaandalia watu njia na kisha wao kuikataa, sasa, sababu ya wao kuikataa ni kwa sababu hakuna kitu mle ndani cha kuipokea. Hakuna kitu cha kuipokea. Mama yangu alizoea kusema, "Huwezi kupata damu katika mboga nyekundu, kwa sababu hamna damu katika mboga nyekundu." Kwa hiyo hamna aina yoyote ya Uzima ndani yao ili kupokea, kwa hiyo hauwezi kupokelewa.

Hiyo ndiyo sababu Mafarisayo walimtazama Yesu usoni moja kwa moja na kumuita "Belzebuli," kwa maana hakikuweko kitu ndani yao cha kumpokea. "Lakini wote alionipa Baba," Yeye alisema, "watakuja Kwangu." Kuna—kuna njia fulani itakayotolewa.

25 Unaweza kuzungumza na watu wakati mwingine mitaani, kuzungumza nao juu ya Bwana,

wanakucheka moja kwa moja. Vema, tunapaswa kufanya hivyo, hata hivyo. Lakini sikilizeni, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu kwanza." Inampasa Mungu kuvuta kwanza. Hapana budi kuwe na Uzima. "Na wote ambao amenipa Mimi, watakuja Kwangu."

Yeye alifanya utaratibu kwa wale wanaotaka kukombolewa. Yeye alifanya utaratibu kwa wale wanaotaka kuponywa. Halafu basi kwa sababu kwamba alifanya jambo hili, linamfanya kuwa mwingi wa rehema, kama ambavyo daima amekuwa mwingi wa rehema. Haina budi kuwa, kama ukikataa Hili, hakuna kitu kilichosalia ila Hukumu, kwa sababu dhambi haina budi kuhukumiwa.

Farao, wakati alipoingia ba—baharini, kama mwigaji, akidhania kwamba angeweza kuingia kama Musa alivyoingia. Musa pamoja na jeshi lake, na Farao na jeshi lake wote pamoja walionekana iliwapasa kuangamia baharini. Bali Mungu, aliye mwingi wa rehema, akafanya mlango wa kutokea kwa ajili ya wana wa Waebrania, (kwa nini?) Kwa sababu walikuwa wakitekeleza wajibu wao, walikuwa wakifuata Neno.

Sasa hiyo ndiyo njia pekee ya kupata rehema, ni kufuata maagizo ambayo Mungu ametupa tufuate. Hiyo ndiyo njia pekee anayoweza kuonyesha rehema, ni wakati tunapofuata yale aliyosema tufanye.

26 Kama vile mjadala mdogo si muda mrefu uliopita, pamoja na mhudumu aliyesema kwamba nilikuwa nikifundisha Fundisho la kimitume katika siku hii. Naamini nilieleza hayo siku moja au mbili zilizopita, au wakati fulani, jinsi alivyosema "Wewe unajaribu kuingiza fundisho la kimitume katika kizazi hiki." Yeye alisema, "Wakati wa mitume ulikoma, pamoja na mitume."

Nami nikamwuliza, "Vema, unaamini Neno?"

Akasema, "Naam."

Nilisema, "Ufunuo 22:18 inasema, ya kwamba, 'Ye yote atakayeondoa Neno moja kutoka kwa Hili, ama kuongeza neno moja Kwake,' si maneno mawili tu; Neno moja, toa Neno moja."

Kasema, "Ninaamini jambo hilo."

Nilisema, "Basi ninaweza kuwaambia mahali ambapo wakati wa mitume ulitolewa, Baraka za kimitume zilitolewa kwa Kanisa; sasa wewe niambie ambapo Mungu aliziondoa Kanisani, kwa Neno. Huwezi kufanya jambo hilo; hakuna." Nikasema, "Sasa kumbuka, ya kwamba Petro, kwenye Siku ya Pentekoste, yeye alikuwa ni—ndiye mwanzilishi wa wakati wa mitume. Naye akawaambia wote, 'Tubuni mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie. '"

27 Sasa kama unataka kusikiliza mlio wa kuku wa kimadhehebu, na kuishi huko nje katika mambo ya ulimwengu, basi inaonyesha ya kwamba kuna kasoro fulani. Kwa sababu, Hilo ni Neno. "Kila atakaye, na aje." Na kama unayo nia, unapaswa kuja. Lakini kama huna nia, basi uko katika hali ya huzuni. Lakini kama una nia ya kuja, njoo ufuate kanuni ya Mungu!

Wala Yeye hashindwi kutimiza yale aliyoahidi. Wakati mmoja nilikuwa kijana, na sasa mimi ni mzee, sijapata kumwona akishindwa katika Neno Lake. Kwa sababu, Yeye anaweza kufanya lolote bali hawezi kushindwa. Hawezi kushindwa. Mungu hawezi. Haiwezekani kwa Mungu kushindwa, na kubaki Mungu. Yeye hana budi kufanya hivyo.

28 Sasa jeshi la Farao lilijaribu kuiga, kwa sababu hawakuitwa wala hawakuwa na Uzima huo. Katika … Ahadi hiyo hakupewa Farao. Ahadi hiyo haikutolewa kwa ajili ya nchi ya ahadi.

Na mtu wa kuiga, akijaribu kumfuata mwamini halisi aliyeitwa hivyo, anafanya tu dhihaka. Hiyo ndiyo shida ya mfumo wetu wa kidini siku hizi, ni watu wengi sana wanaojaribu kumwiga Roho Mtakatifu, watu wengi sana wakijaribu kuiga ubatizo, watu wengi sana wakijaribu kuiga wakati wa mitume. Ni kwa ajili ya waaminio, na hilo pekee. Mungu amefanya njia, mwingi wa rehema, ili kwamba watoto Wake wasiangamie. Yeye amefanya njia kwa ajili yao.

Sasa, Farao akijaribu kufuata, alizama katika maji yale yale yaliyomwokoa Musa na kundi lake. Sasa, Musa hakufa maji, kwa sababu Mungu ni mwingi wa rehema kwao wanaofuata njia Yake aliyoiandaa. Amina.

Mnaweza kuona ninalomaanisha? Kwamba, usiku wa leo, watu wasioamini katika uponyaji wa Kiungu, watu ambao hawaamini ubatizo wa Roho Mtakatifu, wanawezaje kupokea cho chote? Mungu ni mwingi wa rehema kwa wale watakaomfuata; si kwa kufuata kanuni ya imani, bali kwa wanaomfuata Mungu.

29 Mungu ni Neno, nalo lilifanyika mwili na kukaa miongoni mwetu, sasa, ili apate kuzaa zile sifa nyingine za Mungu. Mwili huo, Yesu, ulikuwa ni mwili wa Mungu, sifa. Musa alimwona akipita, sehemu Yake ya nyuma; hakuna mtu aliyeuona uso Wake. Lakini sasa tumemwona, tumemtazama Yeye, tunamwona kama Dhabihu. Sasa, mnaona, Yeye alikuwa ni sifa ya Mungu, ikionyeshwa, lile Neno. Hivyo ndivyo Yeye

alivyokuwa.

Na wakati mwamini ye yote anapomjia Mungu, yeye huwa sifa ya Mungu ya Neno Lake, yeye hutumika kudhihirisha Neno lililoahidiwa kwa ajili ya siku hiyo. Mnaona? Hiyo ni kweli. Mungu, mwingi wa rehema, kamwe hajatuacha bila ushuhuda. Yeye ni mwingi wa rehema.

30 Tunaona sasa ya kwamba Mungu alikuwa na rehema sana kwa Musa huko nje kwenye ile bahari iliyokufa, huko nje katika Bahari ya Shamu kule nje, hasa. Ndipo wakati Yeye aliposema hapa, katika Kutoka 19:4, Yeye alisema, "Nilikuchukua juu ya mbawa za tai, nikakuleta Kwangu. Niliwachukua juu ya mbawa za tai, na kuwaleta Kwangu!" Kulikuwako na watu wengine katikati ya bahari huko nje, pia, wakijaribu kuiga. Lakini ni nini? "Aliwachukua juu ya mbawa za tai."

Sasa Mungu daima huwalinganisha manabii Wake na tai. Na ilikuwa ni kitu gani? Musa alikuwa mjumbe Wake. Nao walikuwa wakimfuata Musa, na hizo zilikuwa mbawa za tai ambazo zilibebwa, kwa sababu alikuwa akibeba ujumbe wa Mungu. Nao watu wakafuata jambo hilo. Walikuwa wakimfuata Mungu walipomfuata Musa na ujumbe Wake wa ukombozi. Na Biblia ilisema ya kwamba, "Yeye, hawakuangamia pamoja na wale wasioamini." Maana, Mungu alikuwa mwingi wa rehema kwao, kwa sababu walikuwa wakifuata amri Zake. Mungu anatutaka tufuate amri Zake.

31 Tungeweza kusema vivyo hivyo kuhusu Kora na kuhusu Dathani na kundi lao la watu wasioamini, walipojaribu kuiga. Walijaribu kuingiza kitu fulani katika mpango wa Mungu. Hawakupenda mpango wa mtu mmoja. Hawakupenda jambo hilo. Iliwabidi kuwa na kitu cha kufanya. Kora alisema, "Mbona, kuna watu watakatifu zaidi kuliko wewe, Musa. Unajifanya kama kwamba wewe tu ndiye pwani kwenye…au ndiwe pekee kijiwe katika pwani, hasa." Kisha akasema, "Mimi—mimi … haukupaswa kufanya hivyo. Na kuna watu wengi zaidi hapa."

Naye Musa alijua ya kwamba alipaswa kuwachukua watoto hao katika nchi ya ahadi, kwa sababu alipewa ahadi. Naye hana budi kuwapeleka kwenye nchi ya ahadi.

32 Na, leo, Roho Mtakatifu yuko hapa kuthibitisha Neno la Mungu, na hilo ni bawa la tai ambalo tunapaswa kupanda juu yake; si theolojia ya kujitengenezea. Bali inatupasa kupanda juu ya mbawa za tai, kwenye Nchi ya ahadi.

Na hapa walikuwa wakienda kuchukua kundi la kuku huko nje, Kora aliwazia, mwajua, kuja huku, kumwiga huyu, yule tai. Na walipofanya hivyo, Mungu alisema, "Jitenge nao," Naye akaumeza ulimwengu. Yeye angalimeza kitu hicho chote, viumbe vyote, bali Mungu alikuwa mwingi wa rehema kwa wale wanaojaribu kulifuata Neno Lake. Daima, Mungu mwingi wa rehema. Wengi wao walikuja upande wa Musa, na Mungu akaifungua nchi na kuwameza wasioamini. Yeye, yule—asiyeamini, daima ataangamia.

33 Wale ambao hawakuamini, ingawa walitoka na kutembea kwa kitambo kidogo, lakini, wao, Yesu alisema, "Wao, kila mmoja wao, amekufa." Mauti ni "kuangamia." Wamekufa. Hebu wazia tu juu yao. Walitoka, wakaona miujiza ya Mungu, wakaona mkono mkuu wa Mungu, wakafurahia mana; kisha wakatoka wakaenda kule na kumsikiliza mtu mmoja jina lake Balaamu, ambaye alipotosha njia ya Mungu, kwa mafundisho yake kinyume cha Neno, "Sisi sote ni ndugu, kwa hiyo hebu sote tuungane pamoja."

Huo ndio mfumo mwingine wa Balaamu unaoinuka, leo, "Hebu sote tuungane pamoja." Haitafaa kitu. Hebu na tuenende pamoja na Tai, Yehova Tai. Ninyi ni tai.

Kuna watatu tu waliookolewa kutoka kwenye kundi lote; Musa, Kalebu, na Yoshua. Hao wengine waliangamia jangwani; Yesu alisema hivyo, katika Yohana Mtakatifu mlango wa 6. Mungu, katika rehema, asingewaacha waangamie, kwa sababu, pamoja na hao wengine wasioamini. Wote walikufa papo hapo jangwani, nao wamekufa. Mungu alimwokoa Musa pamoja na tai waamini, kwa sababu waliheshimu Neno Lake.

34 Na leo, rafiki, njia pekee tunayoweza kupata kibali kwa Mungu; Mungu ni mwingi wa rehema, leo, bali hatuna budi kuheshimu yale aliyosema juu yake. Huwezi tu kuchukua yale mtu mwingine aliyosema. Huna budi kuchukua yale Mungu aliyosema. Yeye alisema, "Neno la kila mtu na liwe uongo, na Langu liwe kweli."

Leo tunaambiwa ya kwamba, "Yote unayopaswa kufanya," katika sehemu nyingi, "ni kujiunga na kanisa, kuwa na kanuni ya imani, ama kitu kama hicho; ama kuomba, ama kuandika jina lako kwenye kitabu, ama kunyunyiziwa ama kubatizwa kwa njia fulani, ama kitu kama hicho. Hilo tu ndilo unalopaswa kufanya." Lakini hilo ni kosa.

Ili uwe tai wa Mungu, huna budi kulifuata Neno, siku baada ya siku. Huna budi kuendelea, kulisha Neno.

35 Sasa tunawaona, baada ya wakati huu, wakinung'unika tena, wamedhoofika katika imani, baada ya Mungu kuwaonyesha rehema. Na tunawapata wakimnug'unikia Mungu, na walipofanya hayo walikuwa

wanakufa kwa kuumwa na nyoka. Vema, walistahili. Hakika walifanya hivyo. Mtu yeyote ambaye angekosea Neno la Mungu na kufanya mambo haya waliyofanya, walistahili kufa. Kila mmoja wao aliyetamani, alistahili kufa jangwani.

Bali walipokuwa hawawezi kabisa na hata Daktari Musa na wengine wao hawangeliweza neno, nao walikuwa wakifariki kwa maelfu; bali Mungu, mwingi wa rehema, alifanya mlango wa kutokea kwa wale ambao wangemwamini. Alitengeneza dawa Yake, kwa kuinua nyoka wa shaba. Mungu katika utajiri Wake … Mungu alifanya njia ya kutokea ili watoto Wake wanaoamini wapate kuponywa.

Mungu anajali kila kitu kilicho kibaya, kila kitu unachotarajia. Kila mwendo wa maisha, Mungu anakujali. Wewe ni mtoto Wake, Naye ni mwingi wa rehema. Anataka kukufanyia.

36 Wale watu walitenda dhambi baadaye, kwa kuchukua kitu kile kile ambacho Mungu aliwafanyia upatanisho, kwa nyoka wa shaba ambaye aliwakilisha dhambi ambayo tayari imekwishahukumiwa, nao wakakifanya kipawa hiki ibada ya sanamu. Na kwa hiyo wakafanya dhambi tena. "Mungu hatashiriki utukufu Wake na mtu ye yote." Kwa hiyo, hatuwezi kuwa na miungu wawili, watatu, wanne. Kuna Mungu mmoja tu. Yeye hatashiriki utukufu Wake na kitu kingine chochote. Yeye ni Mungu, peke yake, mnaona; ili kwamba makafiri wana miungu mingi. Tuna Mungu mmoja, Naye hatashiriki utukufu Wake na mwingine, wala hataruhusu chochote kiwe sanamu mbele Zake. Hata ingawa alikuwa amefanya upatanisho kwa ajili ya watu, na ilikuwa ni Neno la Mungu, ilikuwa ni kweli; bali walipoanza kuabudu jambo hilo, ndipo wakaingia katika shida.

37 Sasa hilo ni jambo lile lile tu, nafikiri, hilo limetukia kwa nyakati zetu za kanisa. Mungu alitutumia ujumbe wa Martin Luther pamoja na ujumbe wake, John Wesley, ujumbe wa kipentekoste, lakini tulifanya nini nao? Jambo lile lile walilofanya na huyo nyoka wa shaba, tulilifanya sanamu, "Mimi ni mfuasi wa *hili*, nami ni mfuasi wa *lile*." Unaona, wewe ni mfuasi wa kitu fulani bila unyofu unaoshikamana na ibada halisi ya Mungu ya Neno.

Ni kitu gani kilichotukia? Biblia, tunaambiwa katika Biblia, ya kwamba, "Nabii alichukua sanamu hiyo na kuiangamiza." Haleluya!

Kile tunachohitaji jukwaani leo ni nabii atakayeiangamiza sanamu ya madhehebu, wanayodhani wanaenda Mbinguni kwa sababu ya kuwa na imani fulani ama madhehebu; inahitaji kuangamizwa na kuteketezwa, kutupiliwa mbali. Mungu amejaa rehema. Yeye ni mwingi wa rehema. Yeye ni mwingi wa rehema. Katika siku ambazo tungekuwa katika mchafuko huo wa giza kule, bali Mungu, mwingi wa rehema, ametutumia Roho Mtakatifu wa kweli hasa, akifasiri Yeye Mwenyewe papa hapa katika jengo hili kila siku. Mungu, mwingi wa rehema Zake, jinsi tunavyomwona kuwa wa ajabu! Naam, bwana.

Sasa yote waliyodhani wangeweza kufanya ni kumwendea tu huyu nyoka, ama kitu hiki kidogo ambacho Mungu alikuwa amekifanya kule nje, alimwambia Musa afanye na kutundika kwenye mti, nao wangeweza kuponywa bila uaminifu wowote. Walisimama tu na kuiangalia. Nao wakaanza kuiabudu, na Mungu akamtuma nabii na kuiangamiza.

38 Sasa, wote waliokataa kumwangalia yule nyoka nyikani, waliangamia. Sasa Mungu hufanya njia, lakini kama unakataa kuiangalia, kama utaketi ng'ambo ya barabara, kama utashikilia kanuni fulani ya imani na kukataa kuangalia moja kwa moja katika Neno na kuona kama ni kweli au la; wote waliokataa kuangalia, waliangamia. Na Mungu ni Mungu asiyebadilika kamwe. Na wote waliokataa kuangalia, waliangamia. Ndivyo ilivyo leo, jambo lile lile.

Ndipo watu wakatenda dhambi baadaye, na kama walivyofanya sikuzote, na kutengeneza sanamu kwa—kutoka kwake, wakifanya a—a—a … kupata, wakijaribu kupata uponyaji bila uaminifu, nao "ni washiriki wa kitu fulani," na jinsi tunavyofanya siku hizi. Na sasa tunaona basi, tofauti yake, ilikuwa, ya kwamba Mungu …

Ulikuwa upatanisho mzuri na ishara nzuri kwa wakati huo. Wakati huo, ilikuwa sawa. Lakini ilikuwa tu iwe kwa ajili ya wakati huo, kwa ajili ya safari hiyo. Hilo tu ndilo litakalofanya kazi, safari *hiyo*.

39 Na ujumbe ambao Martin Luther aliuleta, wa kuhesabiwa haki, ulikuwa sawa kwa wakati wa Luther. Huo ndio umbali wake.

Utakaso ulikuwa mzuri katika wakati wa Wesley. Huo ndio umbali wake.

Ndipo tukaingia katika wakati wa kipentekoste. Na kurudishwa kwa karama ni jambo zuri sana, lilikuwa ni zuri katika wakati huo, bali tunapita zaidi ya hayo sasa. Sisi tumepita hayo, hakika tu kama kuna dunia. Inatupasa tuende mbele zaidi ya kitu hiki, maana tuliyofanya juu ya jambo hili ni kama na hao wengine walivyofanya huko nyuma, yaani kufanya sanamu toka kwake. "Mimi ni mfuasi wa utaratibu huu, mimi ni mfuasi wa utaratibu wake."

Mungu atamtuma mtu ambaye atavunja kitu hicho na kukivunja vipande-vipande, na kulithibitisha

Neno Lake, Neno kamili. Angalia. Mungu asifiwe! Sasa tunaona ya kwamba hiyo ni kweli. Mungu, mwingi wa rehema Zake!

40 Ndipo wakati nabii alipoharibu jambo hili, liliwaacha bila ishara yo yote ya uponyaji, ya upatanisho, kwa sababu sanamu yao iliangamizwa. Lakini Mungu, mwingi wa rehema, aliwafanyia mwingine. Naye alifanya nini, hilo? Yeye alivuruga maji kwenye kidimbwi kwenye hekalu, na wengi wakaja na wakaponywa, kwa kuingia kwenye maji haya. Yesu alishuka kwenye kidimbwi kile kile, na akamwona mtu aliyekuwa amelala pale kwa miaka kadhaa, akingojea kutikiswa kwa maji. Mwone Mungu, mwingi wa rehema! Ingawa walikiabudu kitu hicho, ingawa ilimbidi nabii kukirarua, Mungu alifanya njia nyingine kwa ajili yao, maana Yeye ni mwingi wa rehema. Anawataka waponywe, Naye akafanya njia kwa ajili ya uponyaji wao.

Sasa, basi hilo liliendelea, ulimwengu ukawa wenye dhambi zaidi na wenye dhambi zaidi, wakati wote. Na hatimaye ulimwengu ukawa wenye dhambi sana hata Mungu angaliuangamiza, Yeye alisema katika Malaki 4, "nisije na nikaipiga dunia kwa laana." Angeweza kufanya jambo hilo; swali tu.

41 Lakini basi Mungu, mwingi wa rehema, alimtuma Mwokozi, Yesu Kristo. Alimtuma Yesu kuwa Mwokozi na mponyaji pia. Kwa kuwa Yeye alisema, "Kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka wa shaba jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa," kwa kusudi lile lile. Yeye, ule upatanisho, hilo ndilo tunalodai, si chochote ila ule upatanisho. Kile Yesu alichonunua kwa Damu Yake, hicho ndicho tunachodai. Na Biblia ilisema, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake; na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona." Hilo ndilo tunaloweza kudai, kwa sababu huo ndio ule upatanisho, ambao tunautetea, unaagizwa kwa ajili yetu. Mungu, ni mwingi wa rehema!

Huu ulikuwa uwe upatanisho wa Milele, kwa sababu Yeye alikuja Mwenyewe. Mungu alikuja Mwenyewe, katika umbo la mwili wenye dhambi, kufanya u—u—u—upatanisho wa Milele; na kuteseka katika mwili, na kufanya upatanisho; kisha akarudi katika umbo la Roho Mtakatifu, kuthibitisha huo upatanisho. Ambapo hakuna nyoka wa shaba ama maji ya shida yasingeweza kufanya hivyo, yote yalionyesha ule Upatanisho mkamilifu. Mungu, mwingi wa rehema Zake, amefanya hivi.

42 Sasa, leo, kwa kuwa ndiyo siku tunayoishi, tumepitia katika nyakati hizi za kanisa na kuelezea kila kitu mbali na Hilo. Wanatheolojia wetu wa siku hizi wamepoteza upande huo Wake. Wamelieleza vingine, kwa ajili ya siku zingine, wakati mwingine, mengineyo, mbali sana, wakati mrefu sana uliopita. Na uponyaji wa Kiungu ulikuwa karibu umechezwa, ni vigumu kumpata mtu yeyote ambaye angeuamini. Waliufanyia mzaha. Si zaidi ya miaka ishirini iliyopita, walikuwa wakilidhihaki. Wapentekoste walikuwa wameliacha. Walianza katika siku za mwanzoni, bali waliiacha.

Angalia jinsi walivyofanya. Sasa wana tabia mbaya ya kimadhehebu, wakikimbilia kuwafanyia kila mmoja kanuni ya imani, na kadhalika. iIsipokuwa, badala ya kuikubali Nuru, wakati Nuru ilipoingia; waliunda madhehebu na kujifanyia kanuni za imani, kila mmoja akija, akijifanya fundisho na kudumu katika fundisho hilo. Na ndipo wakaondolewa sana hata Roho Mtakatifu asingeweza kuingia kanisani. Wao wanakuwa tu sanamu nyingine kama nyoka wa shaba, ikawa ni—ni ibada ya sanamu. Kila mtu alisema, "Mimi ni mshiriki wa hili, nami ni mfuasi wa lile." Ilikuwa ni kuabudu sanamu. Tulikuwa katika machafuko yayoje, wakati wa mwisho.

Lakini Mungu, mwingi wa rehema Zake, amemrudisha Roho Mtakatifu juu yetu, na kuthibitisha Neno Lake usiku wa leo kama alivyoahidi angefanya. Mungu aliahidi angefanya mambo haya. Angalia kile alichofanya!

43 Angalia yale aliyofanya, jinsi sasa tunaweza kuona jinsi alivyoahidi kila wakati jambo fulani litukie. Nasi tunaona ya kwamba ilitukia sawasawa kabisa na jambo hilo, ya kwamba Yeye alisema angefanya hivyo, kwa sababu Yeye ni mwingi wa rehema Zake, daima kuwa na rehema kutimiza kila Neno ambalo ameahidi. Hana budi kufanya jambo hilo, na daima, kusudi adumu kuwa Mungu. Daima Yeye hufanya hivi, Neno Lake daima linatimia katika majira Yake. Mbegu Yake ambayo Yeye ameipanda duniani. Yeye alifanya nini? Yeye aliiweka hapa katika Neno, na hiyo ni mbegu. Na kila marai wakati unapokuja, hiyo mbegu huiva, ndipo matengenezo yanatokea. Naye aliahidi jambo hilo, nalo linafanya hivyo.

Sasa hatukustahili mambo haya. Hatukustahili baraka hizi za Mungu, kwa sababu tulikuwa tumeenda kutafuta mambo ya ulimwengu, tukaingia katika kosa la Kaini. Kaini, alijenga madhabahu nzuri, kanisa zuri, na kupamba kwa maua, akidhani kuwa hivyo ndivyo ilivyopasa hasa, "Ni kichala cha matofaa, ama mapera, ama makongomanga, au vyovyote ilivyokuwa," ambayo baba yake na mama yake walikula katika bustani ya Edeni, ikawafanya kufukuzwa. Na kwa hiyo akamtolea Mungu hiyo, naye Mungu akaikataa.

44 "Bali kwa imani Habili alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko ya Kaini."

Na, leo, Biblia ilisema katika Yuda, ya kwamba, "Wameikimbia njia ya Kaini; waliangamia katika maasi ya Kora." Mwaona, "kwenda katika njia ya Kaini," kujenga madhabahu, kujenga makanisa, madhehebu,

wakiyapamba kwa maua, makanisa makubwa, washirika wengi kuliko wengine wao; wakipokea vitu, chochote kinachokuja, na vingine vya kurukaruka, na kushikana mikono, au kubatizwa namna fulani, au kunena kwa lugha, au kukimbia kwenye sakafu na kuandikwa jina kitabuni. Hiyo ni kweli. Na halafu fungua ile Kweli halisi itakayohubiriwa, na kuikana. Inawezaje kuwa hivyo? Angalia jinsi tulivyokuwa katika machafuko! Angalia.

Na Biblia ilisema, "Nao wakaenda katika njia ya Balaamu, wakaangamia katika maasi ya Kora." Waliangamia katika maasi! Kulikuwa na ubishi gani wa Kora? "Mbona, unafikiri wewe ndiwe mtu mtakatifu pekee? Mbona, Mungu … Sisi sote ni watakatifu. Kanisa lote ni sawa. Kila … Sote tunakusanyika pamoja, hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya." Hapo ndipo waliangamia, hapo. Nasi kweli tulistahili. Tulistahili kuwa hivyo.

Lakini Mungu, mwingi wa rehema, ametutoa kwenye machafuko hayo na kuturuhusu tuyaone kabla jambo hili halijatukia hapa. Tajiri katika rehema Zake, na akaturudishia uamsho wa uponyaji wa Kiungu, na kuja tena kwa Nguvu za Mungu. Kulingana na historia, hakuna uamsho uliopata kudumu zaidi ya miaka mitatu. Uamsho huu uliendelea kwa miaka kumi na mitano, umekuwa ni mioto inayowaka moto, kote na kote ulimwenguni. Kwa nini, kwa sababu tulistahili? Mungu, mwingi wa rehema Zake, si kwa kuwa tulipenda hayo, au kwa sababu tulistahili, hasa. Hebu fikiri tu yale yaliyotendwa!

45 Nafikiri juu ya mmoja wa dada zenu papa hapa Phoenix, ambao wengi wenu mnamjua, Bibi Hattie Waldrop, alikuwa na kansa ya moyo. Naye alikuwa kwenye mstari wa maombi hapa wakati mimi na Ndugu Moore tulipokuwa hapa mara ya kwanza, yapata miaka kumi na mitano, kumi na minane iliyopita. Naye alikuwa akifa, kwa kansa ya moyo, naye alipaswa kufa muda mrefu uliopita. Lakini Mungu, mwingi wa rehema, alituma Nguvu Zake juu yake. Naye akayaokoa maisha yake, naye anaishi leo. Mungu mwingi wa rehema!

Mbunge Upshaw, mtu mashuhuri. Nafikiri yeye alikuwa rais, ama kitu fulani, cha—cha Baptisti, Southern Batisti Convention, wakati mmoja, ama makamu wa rais ama kitu fulani. Alikuwa amefanya yote. Alikuwa ni mtu mzuri. Alifanya yote aliyojua jinsi ya kufanya. Alikuwa amekwenda kwa kila daktari. Hakuna mtu angaliweza kumfanyia kitu. Alikuwa amefungwa chini. Wahudumu walikuwa wamemwombea. Alikuwa amemwagiwa galoni moja ya mafuta kichwani mwake, akipakwa mafuta, ya wahudumu mbalimbali kila mahali.

46 Na usiku mmoja, Los Angeles, California, nikipanda kwenye mimbara, nilitazama kundi la magari ya kusukumwa, yapata mara mbili au tatu ya hao wanaoketi hapa yote juu chini roshani, huku na huko. Na halafu kulikuwa na kitanda kilichokuwa na msichana mdogo mweusi ndani yake, msichana mdogo Mnegro, na mama yake—yake alikuwa ameketi karibu naye. Na ndugu yangu alikuwa analeta mstari wa maombi.

Nami nilikuwa nikiangalia, bila kujua kilichokuwa kikiendelea. Nami nikamwona daktari, mwenye miwani ya kobe, akimfanyia upasuaji msichana mdogo wa kinegro, kwa ugonjwa wa koo, naye akapooza. Ndipo nikaangalia kila mahali, nikawaza, "Yuko wapi huyo mtoto?" Sikuweza kumwona.

Baada ya kitambo kidogo, kule chini kabisa, hakuna tumaini, msichana mdogo mzuri mwenye umri wa karibu miaka saba ama minane, apate kupooza maishani mwake mwote. Na kulikuwako na mama yake pale chini kwa magoti yake, akiomba. Ndipo nikasema, "Daktari huyu alimfanyia upasuaji msichana wako mdogo," na nikaeleza.

Akasema, "Hiyo ni kweli, bwana."

Ndipo akajaribu kumpeleka mtoto huyo jukwaani. Walimwambia asifanye hivyo. Walijaribu kumtuliza. Karibu na wakati walipomtuliza, nikawaza, "Vema, tutapata nafasi ya kumwombea." Katika dakika chache … Labda watu papa hapa walikuwa pale usiku huo.

Nami nilikuwa nikiangalia kule kwenye wasikilizaji, nilimwona yule msichana mdogo akishuka kwenda chini, ilionekana kama kupitia kwenye—kwenye barabara ndogo nyembamba, akiwa na mdoli mikononi mwake, akimtikisa yule mdoli. Haijalishi daktari alikuwa amesema mara ngapi kuwa mtoto huyo angalipooza maishani mwake mwote; Mungu, mwingi wa rehema, alimshusha Roho Mtakatifu, kwa ono, na yule mtoto msichana akainuka kutoka pale, naye pamoja na mama yake wakashikana mikono na kutembea kwenye roshani, wakimsifu Mungu.

47 Huko nyuma kule aliketi mzee mmoja, Mbunge Upshaw, wengi wenu mnajua ushuhuda wake. Alikuwa mtu mwema, alijaribu maishani mwake mwote, mgonjwa kwenye kiti cha kusukumia wagonjwa muda wa miaka sitini na sita, akisukumwa kitandani; akiwa na magongo chini ya mikono yake, aliyotembelea, hangeweza kutembea kwa kawaida kamwe. Na hapo aliketi pale, akiangalia jambo hilo. Na ghafla, nikaangalia nje nikaona ono. Huyu hapa anakuja, akitembea juu ya mkutano huo, akiinamisha kichwa chake, angeweza kutembea vizuri kama mtu yeyote. Sikujua mtu huyo alikuwa nani.

Nikasema, "Kuna mtu mashuhuri ameketi kule nyuma. Alianguka kutoka garini alipokuwa mvulana mdogo, akaangukia chuma ya kufungia majani ya ngombe, akaumia mgongo wake. Walitoboa mashimo

sakafuni, kuzuia msukosuko, watu walipotembea, mgongo wake usiumizwe." Nikasema, "Yeye anakuwa mtu mkuu, naye anaendelea kukua zaidi. Yeye ameketi katika duara kuu huko Ikulu."

Ndipo mtu huyu akaja na kuniambia, akasema, "Huyo ni Mbunge Upshaw. Ulipata kumsikia?"

Nikasema, "Sijawahi kusikia habari zake."

Ndipo akampelekea kipaza sauti kule nyuma na walikuwa wakiongea, huku na kule.

48 Ndipo nikaanza kutazama huku na huko, nikamwona yule mzee mbunge akija akitembea kunijia, katika maono, akiwa mzima kabisa kama ambaye hakuwahi kuwa na ulemavu. Mungu, mwingi wa rehema, alimtoa kwenye kile kiti cha magurudumu, naye akatembea bila magongo mpaka siku aliyokufa. Mungu mwingi wa rehema! Wakati madaktari waliposhindwa, wakati sayansi ilishindwa, wakati kila kitu kingine kiliposhindwa, Mungu alikuwa mwingi wa rehema kwa Mbunge Upshaw.

Ninawazia mwenyewe. Kama mvulana mdogo, ninakumbuka kama … Watu wananiita leo, "mchukia wanawake." Sababu yake ilikuwa, ni kwa sababu niliona uasherati mwingi sana kutoka kwa wanawake nilipokuwa mtoto. Niliwachukia. Lakini sivyo nilivyo sasa, najua wako walio wema miongoni mwao. Lakini nakumbuka mambo yalivyokuwa mabaya, uovu mwingi mno. Nami nikawaza, "Jamani, si—sitakuwa karibu na mahali watu walipo. Sina elimu, kwa hiyo sitapata lo lote."

49 Nilipokuwa nikiketi pale nikiwa mtoto mdogo, sikuwa hata na shati, huku koti langu limefungwa *hivi* kwa pini, huku kukiwa na joto jingi. Naye mwalimu akasema, "William, je, husikii joto kwa kuvaa hilo koti?"

Nikasema, "Sivyo, mama, mimi nasikia baridi kidogo." Naye akanilazimisha kwenda kwenye jiko na kuongeza kuni zaidi, jikoni, na nilikuwa karibu kuchomeka. Nami si—sikuwa na shati katika msimu huo mzima.

Ndipo nikawaza, "Iwapo ningalipata fedha, wakati mmoja nikipata kidogo ningenunua bunduki aina ya thelathini—thelathini, ningekuja huku Magharibi na kuishi huku na kuwinda, maisha yangu yote." Sikutaka uhusiano wowote na watu. Nikae tu mbali, kwa sababu hawakunipenda, na—nami ningekaa mbali nao.

Na halafu kila wakati ningeenda mjini, kuzungumza na mtu yeyote, kuwaona jamaa fulani mtaani, niliowajua. Ningesema, "Halo, John, Jim! U hali gani?"

"Loo, habari."

Mnaona, hawakutaka kuzungumza nami, hawakutaka uhusiano wowote nami, kwa sababu ya baba yangu na wale waliotengeneza wiski. Nami si—sikufanya hivyo. Haikuwa chochote nilichofanya. Nami ningalikuwa wa aina hiyo.

50 Lakini sasa nilimwambia mke wangu, si muda mrefu uliopita, "Ukuta wangu umejaa bunduki bora sana zinazoweza kununuliwa." Loo, nami nafikiri juu ya hizo nguo chafu za kale. Usiku wa leo nina suti mbili tatu nzuri. Na hakuna marafiki? Sina budi kujificha huko nyikani, kujiepusha na watu. Kuna nini, ni kwa sababu ya utu wangu, ni kwa sababu ya elimu yangu? La. Mungu, mwingi wa rehema, aliniona katika hali hiyo Naye akaniokoa.

Ninakumbuka nikiongozwa kwa kushikwa mikono, kama kipofu. Sikuweza kuona. Kila kitu mbele yangu kilikuwa ni ukungu; Ningekuwa kipofu maishani mwangu mwote. Lakini Mungu, mwingi wa rehema, alinirudishia kuona. Nina umri wa miaka hamsini na mitano, na bado nina macho mazuri. Mungu, mwingi wa rehema, ndicho kitu pekee ninachoweza kusema.

51 Wakati mmoja kanisa halikuwa na njia iliyoandaliwa ya uponyaji. Walikuwa na moja, bali waliikataa. Lakini Mungu, mwingi wa rehema, amewatumia karama ya uponyaji wa Kiungu. Huyo ni Roho Mtakatifu miongoni mwetu, akilithibitisha Neno kwa ishara zinazofuata. Mungu mwingi wa rehema!

Nina kurasa mbili ama tatu hapa za maandishi haya, lakini sitajaribu kuyagusa, kwa sababu nina—ninajua ya kwamba karibu wakati wa kuanza mstari huo wa maombi umekwisha. Lakini Mungu mwingi wa rehema Zake!

Wengi wenu hapa usiku wa leo, madaktari waliwakataa. Kuna watu wanaoketi kwenye viti hivyo vya magurudumu, labda hawatatoka mle. Hawatatoka humo. Baadhi yao, wamepooza kwa njia mbalimbali, wao (wasingeweza kamwe) wasingeweza kutoka, hakuna njia kwao kutoka. Lakini Mungu, mwingi wa rehema Zake, ametoa upatanisho. Usiukatae. Upokee. Kuna watu huko nje walio na ugonjwa wa moyo, kuna watu walio na kansa, ambao madaktari hawawezi kufanya kitu nao. Huna matumaini, huna msaada, katika ulimwengu huu.

52 Lakini Mungu, mwingi wa rehema Zake, amemtuma Roho Mtakatifu, na yuko papa hapa sasa kuthibitisha Neno, kuthibitisha ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Kwa sababu tunastahili? Kwa sababu Mungu ni mwingi wa rehema Zake! Amina. Sasa huyo Ndiye, yule Mtu, huyo ni Bwana Yesu.

Yeye hajafa, bali amefufuka katika wafu, Naye yu hai milele.

Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele, angali ni mwingi wa rehema Zake kama alivyokuwa kwa mwanamke aliyekuwa akitokwa na damu. Naye akaanza kupitia kwenye umati. Hakukuwa na matumaini kwake, madaktari walikuwa wamefanya yote wangeweza kufanya. Alikuwa akitokwa na damu. Alikuwa anakufa. Naye aligusa vazi la Bwana. Mungu, mwingi wa rehema, aligeuka na kumwambia hali yake. Naye aliponywa ugonjwa huu wa damu.

Maskini kahaba mmoja mchafu alikwenda kisimani siku moja, kuchota maji. Hakuna tumaini. Alikuwa ametengwa na wanawali, kutoka kwa watu, maisha yake hayakuwa mazuri. Naye akawaza, "Kuna faida gani kujaribu? Nimefukuzwa, hakuna kitu kilichosalia kwangu." Lakini yeye aliangalia, amesimama pembeni, ama ameketi kando ya kisima, na kulikuwa na Mtu aliyeketi pale Ambaye alimwambia mambo yote ambayo amewahi kufanya, Mungu mwingi wa rehema Zake.

Mungu yuyo huyo, usiku wa leo, ni mwingi wa rehema Zake, na ni kama tu vile alivyokuwa katika siku hizo. Mungu tajiri. [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.]

53 Nafikiri tuna kadi mia mbili za maombi hapa, au wale tuliokwishawaita ni mia mbili. Tutawaita na kuwaacha watu wajipange. Tutawaombea.

Lakini kabla hatujafanya hivyo, huenda ikawa kuna wageni hapa, ondokeni kwenye ushirikina wote. Huu si ushirikina. Ni udhihirisho wa ahadi ya Mungu. Inategemea unaangalia nini. Hakuna nguvu katika mtu ye yote. Hakuna nguvu ndani ya mtu ye yote. Lakini sisi kama waaminio tuna mamlaka; si uweza, bali mamlaka.

Mtu fulani aliniuliza, si muda mrefu uliopita, kasema, "Ndugu Branham, unaamini una uweza wa kufanya jambo hili?"

Nikasema, "Sina uweza, hata kidogo, bali nina mamlaka." Kila mwaminio anayo. Kama ukiyakataa, utabaki mahali ulipo. Lakini kama utakubali, utafanya mambo makuu sana, kwa maana Mungu ni mwingi wa rehema Zake.

54 Mchukue polisi mdogo anayesimama hapa nje mtaani, nguo zake zikining'inia nusu, yeye ni mwembamba sana. Kofia hiyo imevuta masikio yake chini. Naye atembea ambapo motakaa zinakuja barabarani mwendo wa maili hamsini kwa saa, mwendo wa nguvu za farasi mia tatu. Yeye hana nguvu za kusimamisha baiskeli. Hiyo ni kweli. Lakini hebu acha tu apige filimbi hiyo na kuinua mkono huo, na uangalie breki zikilia. Yeye hana uweza, bali ana mamlaka. Mji wote uko nyuma yake.

Na wakati mwanamume au mwanamke, si hoja uko katika hali gani, unayo mamlaka kutoka kwa Mungu, kwa ahadi, kwa sababu Yeye ni tajiri na ametuahidi kutufanyia mengi mno. "Kama ukiuambia mlima huu, 'ng'oka, 'wala usitie shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba yale uliyosema yatatimia, unaweza kupata yale uliyosema." Huna uweza, bali una mamlaka.

Kumbuka wakati Yeye aliponiambia kule nyuma, kasema, "Utaweza kufunua siri za mioyo." Kwa kuwa Yeye … Mnakumbuka jambo hilo, wengi wenu ninyi watu wa Phoenix? Yeye aliahidi jambo hilo. Yale anayoahidi, Yeye hufanya.

55 Sasa kuna baadhi yenu hapa ambao hawana kadi za maombi, na hapana shaka. Ni wangapi walio wagonjwa na hawana kadi za maombi, inueni mikono yenu? Hakika. Vema. Kama unataka kujua, si mamlaka … si nguvu, bali mamlaka ya Neno, "Mambo nifanyayo, ninyi nanyi mtayafanya."

Yesu aliahidi, katika Luka 17:30, ya kwamba kabla tu ya Kuja Kwake, kungekuwako na kama wakati wa Musa … ama Nuhu, "Walipokuwa wakila na kunywa, na kuolewa; wala hawakujua hata siku ile Nuhu alipoingia katika safina." Yeye alisema kungekuwa na wakati huo. Ndipo akasema pia, "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu," na akasema, "haya yatatukia katika siku ile atakapofunuliwa Mwana wa Adamu, atakapofunuliwa Mwana wa Adamu katika siku za mwisho."

56 Sasa angalia kile Yeye, jinsi Mwana wa Adamu alivyojifunua katika nafsi ya Malaika huyu, ambaye alikuwa ni Mwana wa Adamu. Kabisa. Ibrahimu alimwita, "Elohimu." Yeye alikuwa Mwana wa Adamu, akajifunua kabla tu ya ulimwengu wa Mataifa kuchomwa moto. Yeye alifanyaje jambo hilo? Kwa mwaminio. Kwa wajifanyao waamini, aliwatumia wahubiri wawili chini huko kuwahubiria. Lakini kwa mwamini halisi, Yeye alisimama ameelekeza mgongo Wake hemani, Naye akasema, "Ibrahimu." Yeye alikuwa Abramu siku ile … siku chache zilizopita, hiyo. Lakini sasa yeye ni Ibrahimu. "Yu wapi mkeo, Sara?"

Kasema, "Yumo hemani, nyuma Yako."

Kasema, "Nitatimiza ahadi Yangu kwako. Nitawatembelea."

Loo, Ibrahimu alikuwa na umri wa miaka mia moja, na Sara alikuwa na tisini; bali Mungu, mwingi wa

rehema, alitimiza ahadi Yake. Ikamleta mtoto mchanga, maana Mungu ni mwenye rehema, Naye ni mwingi wa rehema. Yeye ni mwingi wa rehema. Yeye hutimiza ahadi Yake.

57 Angalia, huku mgongo Wake umeelekezwa hemani, Sara akacheka na kusema, "Mambo haya yangewezekanaje? Mimi ni mzee. Ninawezaje kupata raha na mume wangu, kama kijana mwanamke aliyeolewa? Mbona, yeye ana umri wa miaka mia moja. Uhusiano wetu wa mume na mke ulikoma miaka mingi, mingi sana iliyopita. Hili lingewezekanaje?" Naye akacheka juu ya jambo hilo.

Ndipo yule Malaika akiwa na … Mwana wa Adamu ameelekeza mgongo wake kwenye—kwenye hema, akasema, "Kwa nini Sara akacheka, akisema, 'Mambo haya yawezekanaje?'"

Ilikuwa ni kitu gani? Yesu alisema 'katika Luka Mtakatifu 17:30' kuwa, "Katika siku kama ilivyokuwa katika siku za Lutu," hali ile ile, kabla ya ulimwengu wa Mataifa kuchomwa moto, Alisema, "Mwana wa Adamu atajifunua Mwenyewe katika siku hiyo." Yeye aliahidi ya kwamba ahadi za Malaki 4 zitatimizwa. Ujumbe ungekuja ambao ungewarudisha watu kwenye Ujumbe wa asili wa kipentekoste, na kwa baraka zile zile walizopata kwenye siku ya … Ni kitu gani? Ni tai mwenye mabawa mawili, Agano Jipya pamoja na Agano la Kale, kukusanya ahadi zake pamoja, za Mungu, kutimiza ahadi za Biblia ilivyosema kwamba zitakuwa. Amina.

58 Mungu, mwingi wa rehema, asingewaacha watu Wake watoke katika hili la kimadhehebu, "matajiri katika mali na mambo ya ulimwengu," Wakati wa Kanisa la Laodikia, bali Yeye angefanya njia ya kutokea. Aminini, enyi watu. Mungu akubariki. Amina. Mungu mwingi wa rehema! Rehema za Mungu, hicho ndicho kitu pekee ninachotaka. Si haki Yake, si sheria Yake; bali rehema Yake ndiyo ninayoitaka. Mungu anirehemu. Sote tunajisikia hivyo.

Nilikuwa nikiangalia. Kuna maskini mwanamke mmoja anayeketi hapa nje mwisho wa kiti. Je! Una kadi ya maombi huko nje, mama? Hamna. Hebu niwaonyeshe Mungu ni mwingi wa rehema. Umekuwa na wasiwasi sana hapa siku za hivi karibuni, sivyo? Mbaya sana, na macho yako yamekuwa mabaya zaidi. Hiyo si ni kweli? Hiyo ni kweli. Sasa watabadilika. Mungu, mwingi wa rehema Zake, kwa kukuuliza kama ungeamini hili. Sasa huna kadi ya maombi, huna kitu; bali huhitaji. Mnaona, ni neema uliyopewa.

59 Huyo hapo ameketi mtoto mdogo anayeketi papo hapo mbele, akiwa na namna fulani … ameketi papa hapa. Yeye anaugua uvimbe mwilini mwake. Umeingia pale majuzi tu, majuzi. Hiyo si ni kweli, bwana? Hiyo ni kweli. Hujui ni kitu gani. Unaiogopa. Hiyo ni kweli. Ulisababishwa na jeraha, sivyo? Una kadi ya maombi? Huna kadi ya maombi. Huhitaji moja. Mungu mwingi wa rehema Zake!

Loo, ndugu, dada, mwamini Mungu! Usimtilie shaka. Mwamini Yeye! Hiyo ni kweli.

Huyu hapa ameketi mwanamume, mwenye suti ya kijivu, amevaa miwani. Angalia hapa, bwana. Unaamini? Mungu ni mwingi wa rehema Zake. Umeketi pale na ngiri. Je! Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuponya hiyo ngiri na kukufanya mzima? Ameketi papa hapa mwishoni mwa kiti, akiniangalia. Kama unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuponya hiyo ngiri, Mungu atakufanyia jambo hilo kama utalikubali. Mnaamini jambo hilo? Utakubali jambo hilo? Vema. Unaweza kupata kama utaamini tu, pokea rehema. Naam, bwana.

60 Huyu hapa mama anayeketi hapa nje, anaugua ugonjwa wa mzunguko wa damu mwilini mwake. Lakini kama ataamini, Mungu atamponya, kama akiamini. Ninaamini atalikosa, hakika kabisa. Nirehemu, ndilo ombi langu. Ningeweza kuona kidogo mwanamke huyo … Bibi Riley, unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuponya mzunguko huo mbaya? Kama ukipenda, lipokee! Amina. Amini tu. Mungu ni mwema, sivyo, Stella? Naam. Hiyo ni kweli. Sijapata kumwona mwanamke huyo maishani mwangu. Lakini, Mungu, katika rehema Yake!

Huyu hapa ameketi mwanamke mwingine, ameketi moja kwa moja nyuma kule, moja kwa moja nyuma, akiniangalia moja kwa moja. Yeye, pia, ana mzunguko mbaya wa damu, pia. Alikuwa akiwazia jambo hilo wakati huo tu. Sijapata kumwona mwanamke huyo maishani mwangu. Kwa kuwa mwanamke huyu mwingine alikuwa na jambo lile lile, niangalie. Unaniamini mimi kuwa nabii wa Mungu, ama mtumishi Wake? Pia una ugonjwa wa moyo. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Huna hiyo sasa. Mungu, mwingi wa rehema Zake, anaonyesha ya kwamba Yeye yu hai hapa jengoni usiku wa leo. Mungu mwingi wa rehema Zake! Amina.

61 Ingewezekana kuwe na, ni wenye dhambi wangapi na waliorudi nyuma wangesimama kwa miguu yako, na kusema, "Mungu, mwingi wa rehema Zake, unirehemu"? Simama kwa miguu yako. Nitakuombea, kama unaamini ya kwamba Yeye anataka … unataka rehema sasa. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki, wewe. Ewe uliyerudi nyuma, simama kwa miguu yako. Mungu mwingi wa rehema Zake! Je! Wewe—wewe …

Hakika hujapata kufa ganzi sana, katika hali hii, hata huwezi kuona ya kwamba hiyo ndiyo ahadi yenyewe ya wakati huu. Hakika hujafungwa sana katika madhehebu, na mambo mengine, hata huwezi kuona ya kwamba hii ndiyo ahadi ya wakati huu, Mungu mwingi wa rehema.

Ye yote uliyekuwa, uliyesimama, nitaomba katika dakika moja tu. Ninawatakeni mwende kwenye kanisa zuri la Injili na—na m—mkabatizwe katika ubatizo wa Kikristo, Mungu awape Roho Mtakatifu.

62 Je kuna mwingine ambaye atasimama, na kusema, "Mimi, nataka kukumbukwa. Mungu, katika rehema Zako, nikumbuke. Sijaishi jinsi ningepaswa kuishi. Labda …"? Mungu akubariki, mama. Na Mungu awabariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hiyo ni kweli. "Mungu, mwingi wa rehema Zake, unirehemu." Mungu akubariki, dada. Kuna …

Ni wangapi wengine walio humu ndani, waseme, "Nitasimama. Ninataka Mungu ajue ya kwamba ninataka rehema. Sijaishi vizuri. Nimeishi *hivi* na *vile*. Nimekuwa nikienda huku na huku, bali ninataka rehema Yake." Mungu akubariki, ndugu. Mtu mwingine, aseme, "Mungu mwingi wa rehema Zake!" Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki, dada. Hiyo ni kweli. Mungu mwingi wa rehema Zake! Mungu akubariki, pia. Mungu akubariki huko nyuma. Mungu anakuona. Simameni tu kwa miguu yenu.

Sema, "Je, yafaa, Ndugu Branham?" Hakika. Simama uone ni tofauti gani.

Kama kweli wewe ni mwaminifu moyoni mwako, Mungu ni mwingi wa rehema. "Yeye hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikie toba." Mungu mwingi wa rehema Zake! Ee Mungu, uturehemu.

63 Sasa ni wangapi hapa ndani sasa, ambao wanashikilia hizo kadi za maombi? Walikuwa nini? A na B, sivyo? A na B. Watu wote walio na kadi za maombi A, simameni upande huu, na kadi ya maombi B mtasimama nyuma yao.

Sijui kama kuna baadhi ya wahudumu hapa ambao wangetaka kutarajia kunisaidia. Kama wako, ningependa kuja hapa, ningefurahi kupata msaada wenu—wenu hapa, kwa kuwa tutafurahi kuomba, na kuomba—kuomba pamoja nanyi.

Hii, Biblia ilisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Naam, bwana. "Katika Jina Langu watatoa pepo, watanena kwa lugha mpya." Tumefanya jambo hilo? Kwa neema ya Mungu; si sisi, bali Mungu mwingi wa rehema kulitimiza Neno Lake. Mungu!

Sasa, viti vya magurudumu, kama unataka kuviweka moja kwa moja hapa chini mbele; tutawaombea papa hapa, haitatubidi kuwavuta kupitia kwenye hayo, marefu yote ya kanisa kule. Hebu, vema, hebu waje moja kwa moja hapa. Tutaomba kwa ajili ya kila mmoja, bila shaka. Mungu mwingi wa rehema Zake!

64 Ungeweza kusimama upande wa kulia sasa, kwa dakika chache? Je! Ndugu Brown alikuja pamoja nawe? [Ndugu fulani anasema, "Kuja kesho." - Mh.] Anakuja kesho. Ni—ni—nilikuwa na matumaini angekuwa hapa. Yuko wapi, Ndugu Outlaw yuko wapi, Ndugu Fuller yuko wapi? Baadhi ya hao watu waliokuwa hapa pamoja nami nilipokuja mara ya kwanza, hebu turudi. Mnakumbuka mistari hii ya maombi ya mtindo wa kale, wakati tulipokuwa tukisimama pale hata ingewalazimu kunishikilia upande mmoja, na mtu mwingine upande mwingine, ningekuwa mdhaifu sana?

Ni wangapi wamekuwa katika mikutano hiyo huko nyuma kabisa? Angalia hapa. Mnakumbuka kule nyuma, niliwaambia ya kwamba Bwana Yesu aliniambia ya kwamba, kama ningekuwa mwaminifu, ya kwamba mambo haya yangetukia. Hiyo ni kweli? Hatukuwahi kuwa na kitu kama hicho katika siku hiyo. Lakini ilitukia, kwa sababu Mungu ni mwingi wa rehema Zake, na ni mwaminifu kwa ahadi Yake. Amina! Kujaribu kuondoka, nami siwezi. Amina! Mungu asifiwe! Haleluya! "Loo, nina furaha sana mimi ni mmoja wao!" Amina. Loo, jamani!

> Kuna watu karibu kila mahali,
> Ambao mioyo yao yote imewaka moto
> Kwa Moto ulioshuka juu ya Pentekoste,
> Hilo liliwasafisha na kuwafanya wasafi;
> Loo, linawaka sasa moyoni mwangu,
> Loo, utukufu kwa Jina Lake!
> Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao.

65 Loo, mimi, mnyonge, mwenye mashaka, maskini kipofu, kama nilivyokuwa; na sasa kwa rehema Zake, rehema Yake kuu, ninaweza kuuona Ufalme wa Mungu. Amina. Jinsi Amri Zake zilivyo nzuri!

Simama moja kwa moja, ndugu yangu, kwa mkongojo wako. Kama huwezi kusimama, vema, simama papa hapa, tutashuka moja kwa moja na kukuombea.

Na sasa hebu zile A na B, za kadi za maombi, zijipange upande ule mwingine, nasi tutawaombea.

Ndugu wahudumu, hakika ninyi, kama mnaamini katika kuweka mikono juu ya wagonjwa, njoni papa hapa na kusimama pamoja nami kwenye jukwaa hili. Tutawaombea wagonjwa.

66 Sasa kwenu ninyi watu mliosimama kwenye mstari ule, kama mnaweza kuamini Uwepo wa Mungu upo hapa, kwamba Roho Mtakatifu yupo katikati yetu sasa, akifanya yale hasa aliyosema angefanya. Kama ningekuwa na nguvu za kukuponya, bila shaka ningefanya hivyo. Kama ningalikuwa na njia yo yote ya

kukuponya, bila shaka ningefanya hivyo. Sina. Mimi … Mungu ametoa karama ndogo.

Mimi si mhubiri sana. Sina elimu ya kutosha kustahili kuwa mhubiri, katika hali ya uhubiri wa kisasa, ambapo—ambapo ujuzi unapaswa kuwa ujuzi wa kitheolojia, na lazima kuwa na shahada ya juu, na kadhalika. Siwezi kustahili jambo hilo. Lakini Mungu, akiuona moyo wangu, na kujua ya kwamba ninataka kumfanyia jambo fulani, ninataka kulithamini.

67 Mtu fulani aliniambia hivi majuzi, kasema, "Nafikiri wewe ni mtu mzuri tu, Bw. Branham, lakini ninaamini umekosea kabisa. Wewe uko nje kabisa ya nia. Unajua utahukumiwa mwishoni?"

Nami nikasema, "Angalia, ninataka kukwambia jambo fulani. Nataka kusema kwamba wewe—wewe ungekuwa umesema kweli, kama kusudi lako ni kwa ajili ya ubishi tu. Kama mimi nimekosea, nami si—siamini kwamba nimekosea; lakini kama ningekuwa nimekosea, na nikafahamu sasa hivi kuwa ningeishi kufikia umri wa miaka mia moja, na mwishoni mwa maisha yangu angenihukumu, na aniambie, 'William Branham, Hustahili kuingia katika Mbingu Yangu. Tokeni kwenye giza la nje.' Unajua nini? Ningemtumikia kila siku ya maisha yangu mpaka niende, kwa vyovyote vile. Kwa maana nimepokea mengi sana ya baraka Zake zisizostahiliwa, kwamba Yeye ni zaidi ya uhai kwangu. Yeye ni kila kitu ambacho mimi …"

68 Yote mimi niliyo, yote ambayo ningalitumainia kuwa, nimepata kutoka kwa neema Yake na rehema. Nilikuwa mnyonge, mwenye mashaka, maskini, kipofu; bali kwa neema ameniponya, nami ni mwenye nguvu na mwenye afya, kwa neema ya Mungu. Nina macho mazuri. Nimekula, kunywa, nina kila ninachohitaji. Kamwe hakuahidi kunipa haja zangu; mahitaji yangu.

Na kama nikitupwa mbali siku hiyo, nami nilijua … Siwezi kuona mahali ningekuwa. Lakini kama nilijua ya kwamba nilikuwa nimekosea, na Mungu amenichagua mimi kuwa ni mkosaji, ningetaka kubaki nikikosea, na kwa sababu ninataka kufanya mapenzi Yake. Ni, ninampenda mpaka ninataka mapenzi Yake yatendeke. Sasa, hilo ni tamshi kubwa, bali natumaini mnalipata, katika roho ninayozungumzia ndani yake. Mnaona, ninataka kufanya mapenzi Yake. Ningemwomba neno fulani wakati mmoja, Naye akatikisa kichwa Chake na kusema "hapana," ningefurahia sana hilo kama tu wakati anaposema "ndiyo." Kwa sababu, daima tunapaswa kuuliza, "Mapenzi Yako na yatendeke." Vichwa vyake ni kama tu … kama hayo ni mapenzi Yake, hayo ni … Ni bora zaidi kuliko ndiyo Zake, ikiwa ni mapenzi Yake kufanya hivyo. Hapo ndipo unapompenda kweli. Amina.

69 Nikianza kuzungumza juu Yake, siwezi kuacha tu. Loo, Yeye ni halisi sana, halisi sana kwangu! Marafiki, Yeye—Yeye ndiye yote niliyo mimi, yote ninayoweza kuwa, yote ninayotarajia kuwa, yamewekwa msingi katika Kristo Yesu, Neno Lake.

Ninashukuru usiku wa leo kwa ajili ya ushuhuda wa Roho Mtakatifu, kwa ajili ya Ujumbe. Ninajua huenda, wengine huenda wasikubaliane Nalo, lakini kama nilivyowaambia, nina wajibu wa Ujumbe. Ishara ilitokea, na Mungu hatumii ishara kuonyesha tu ya kwamba Yeye ni Mungu. Ujumbe, Sauti daima huifuata ishara. Kila mtu anajua jambo hilo.

Yesu alikuja na ishara na maajabu. Yeye alikuwa ni Mtu mashuhuri wakati alipokuwa akifanya ishara na maajabu, bali alipoanza kuketi chini na kuanza kuleta Ujumbe, "Mimi na Baba Yangu ni Mmoja," loo, jamani, hilo lilikuwa kosa kwao. Mnaona? Lakini ilibidi Sauti iifuate ile ishara.

70 Musa alipewa ishara mbili, na kila ishara ilikuwa na sauti. Hiyo ni kweli. Nilihubiri juu yake hapa wakati fulani uliopita, mahali fulani, juu ya, *Sauti Ya Ishara*. Lazima iwe na—- na Sauti ya ishara. Ni kubadilika. Daima ni hivyo. Kama sivyo, basi halikutoka kwa Mungu.

Kama mtu akitoka na huduma isiyo ya kawaida, ambayo inapatikana katika Biblia kuwa ni Kweli, na mtu huyo anakaa moja kwa moja katika fundisho hilo hilo la kale la kimadhehebu, sahau hilo. Hakuna kitu kwake! Mungu hafanyi jambo kama hilo. Kitu hicho ni mana iliyooza, iliyo na mchwa, au mabuu, ama vyovyote unavyotaka kuviita, tangu miaka arobaini, hamsini iliyopita, akijaribu kula ile mana iliyoanguka miaka mingi sana iliyopita. Nao wana wa Israeli, safarini mwao, mana mpya ilianguka kila usiku. Hiyo ni kweli, usingeweza kuizuia.

Hatuishi katika wakati mwingine uliopita. Tunakula Mana mpya, Mana mpya kutoka Mbinguni, katika safari yetu tunapoendelea.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa.

71 Bwana Mungu, Wewe ni halisi sana, Uwepo Wako. Ninafikiria juu ya neema, Bwana. Tu—tumeona tu Wewe ukifanya mambo mengi sana! Tumekusikia ukinena kwa lugha, tukikuona ukifasiri, kupitia kwa watu Wako. Ee Mungu, kukuona Wewe ukiponya wagonjwa, kuyafungua macho ya vipofu, kuwafanya viwete watembee, viziwi wasikie, bubu kuzungumza, Wewe ni Mungu mkuu na mwenye nguvu jinsi gani!

Na halafu kuona ya kwamba Wewe uliahidi jambo hili katika siku za mwisho. Ingawa tuna waigaji wa kimwili, bali haya yatangaza tu kwamba kuna Mungu halisi mahali fulani, aliye wa kweli kabisa. Nami

ninaomba, Baba wa Mbinguni, usiku wa leo, ya kwamba tutamjua Mungu sana hata tunaona ya kwamba Wewe upo hapa.

Na watu hawa kwenye mstari, wanapopitia kwenye mstari huu, Bwana … kwa kuwa tunafanya jambo hili kwa sababu, kwamba tuliwapa ahadi. Nawe ulisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

Hawa hapa ndugu wahudumu wamesimama hapa, watu ambao umewachagua, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kuwa vile walivyo usiku wa leo. Ulijua, kabla hakujakuwako na ulimwengu, ya kwamba tungesimama hapa usiku wa leo, kwa sababu Wewe hauna kikomo.

72 Kwa hiyo tunaomba, Baba wa Mbinguni, usiku huu, kwamba hawa wagonjwa, viwete, vipofu, vilema, wenye kansa, chochote kile, wanapopita kwenye msitari huu, hebu wafahamu kwamba Mungu Yule Yule anayejua siri ya mioyo atawaponya iwapo wataikubali, watazame tu na kuelewa.

Yule mtu aliyemwangalia yule nyoka wa shaba kama tu kuhani … kipande cha shaba, hangeponywa kamwe, kwa sababu hakuwa na ufahamu wa kwamba ilikuwa ni kitu gani.

Na leo, Bwana, vivyo hivyo. Kama wakiangalia karama, kuwazia huenda ikaweza kuwasaidia, hawana ufahamu. Liko kwenye uthibitisho wa Uwepo wa Mungu uliopo hapa kuponya. Tujalie, Baba. Jalia litendeke, katika Jina la Yesu. Amina.

73 Nataka kijana mmoja mpiga kinanda, mwanamume au mwanamke akipenda, yeyote yule, aende pale na kupiga wimbo huu, "Ni Tabibu wa karibu, Tabibu wa ajabu," akipenda, popote mpiga kinanda alipo. Sasa hiyo ni …

Ninakumbuka moja ya ibada yangu ya kwanza ya uponyaji, Fort Wayne, Indiana. Msichana mdogo wa Ki-Amishi alikuwa ameketi, akipiga kinanda, "Ni Tabibu wa karibu, Tabibu wa ajabu. Mtoto mchanga aliletwa kwangu jukwaani, alikuwa kiwete. Na nilipokuwa nikimwombea huyo mtoto mchanga, aliruka kutoka mikononi mwangu na kukimbia mbio jukwaani. Yule mama akazimia. Yule bibi akatupa leso yake, akaanza kulia.

Na maskini msichana huyu wa Kiamishi sasa, bila kujua lo lote kuhusu Wapentekoste, kwa sababu alikuwa mfuasi wa kanisa la Kiamishi; bali alikuwa akicheza. Nywele zake ndefu zikaanguka chini; aliinuka katika Roho na kuanza kuimba kwa lugha zisizojulikana, na … na kwa upatano wa wimbo huo. Na kile kinanda kikaendelea kujipiga chenyewe, kikiimba, "Ni Tabibu wa Karibu, Tabibu wa Ajabu." Amina! Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

74 Sasa hebu na tuombe sasa kama … Sasa hebu na kila mtu huko nje aombe. Ninyi watu mnaopitia kwenye mstari, tunapoweka mikono juu yenu, kumbukeni, Yesu alisema, "Kama mngeamini jambo hilo, mtapona." Unaamini jambo hilo? Sasa hebu na tuimbe wote sasa.

Yule Tabibu mkuu sasa yu karibu,
Yesu mwenye huruma,
Ananena … (Hebu tufunge tu macho yetu sasa tunapoimba) … mioyo ya kuchangamka,
Loo, sikieni sauti ya Yesu.
Neno tamu zaidi katika wimbo wa maserafi,
Jina tamu zaidi ya yote yatamkwayo na wenye mwili,
Tamu zaidi … (Baba Mungu, tembea juu ya watu sasa) … kuimbwa,
Ewe Yesu, Yesu mbarikiwa.

"Mkuu …" Sasa unapopitia hapa sasa, Yeye yupo hapa. Aminini ninayowaambia, ama aminini wenyewe, Yeye yuko hapa. Kila mtu katika maombi huko nje sasa kwa ajili ya watu.

75 [Ndugu Branham na wahudumu wanawaombea wagonjwa wakati Ndugu Borders anaongoza kusanyiko katika kuimba. Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.]

Ewe Bwana, naamini; Ewe Bwana, naamini;
Mambo yote yanawezekana, Ewe Bwana, naamini.

Wote wanaoamini, inua mkono wako juu namna *hii*, useme, "Naamini." [Kusanyiko linasema, "Naamini." - Mh.]

Hapa ameketi mtu huyu. Sababu yangu ya kunena naye sana, yeye anakufa kwa kansa. Yeye anatumia mkongojo huu. Hakuna njia ulimwenguni kwa mwanadamu kuishi, nje ya Mungu. Yeye ana kansa tumboni mwote, na atakufa isipokuwa kwa rehema Zake Mungu. Nami ningetamani ninge … [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.] … Neno la kumtia moyo mtu huyu.

Wewe, unajua madaktari hawawezi kukusaidia kitu sasa. Umepita hayo, unaona. Nawe unaninii … Una nafasi moja tu, na hiyo ni katika Kristo, unaona. Na, ndugu, wewe … Nitakufa siku moja, pia. Itakubidi kwenda, kama Yesu akikawia. Sina budi kukutana nanyi kule, kusimama pale kwenye Hukumu. Na usiku

huu …

76 Wajua, kama ilivyo kwenye televisheni, televisheni huchukua hilo kila mara hata tunapojongeza vidole vyote, cho chote kile, kinarekodiwa. Kila neno tunalosema, liko kwenye kumbukumbu. Sasa, unaona, televisheni imethibitisha jambo hilo. Naam, televisheni haitengenezi picha, huelekeza tu wimbi hilo kwenye televisheni. Mnaona, haifanyi hivyo. Kulikuwako na televisheni wakati Adamu alipotembea duniani, kulikuwa na televisheni wakati—wakati Musa alipopitia Bahari ya Shamu, kulikuwa na televisheni wakati Eliya alipokuwa kwenye Mlima Karmeli, mnaona, lakini sasa hivi waliigundua. Mnaona? Na sasa kila mahali mimi …

Kila hatua tunayofanya, na kila sauti, inacheza rekodi itakayokutana nasi Hukumuni. Kila tendo tunalolitenda tutalikuta kule. Sina budi kujibu kwa maneno ninayowaambia, kama mhudumu. Sina budi kufanya hivyo, kwa maana Mungu ataniwajibisha kwa jambo hilo.

77 Basi kama ningaliweza, ningekuponya; kwa sababu umebakiza wakati mdogo, kama isingalikuwa kwa ajili ya Mungu. Sasa, nimeshuka na kuwaombea, yote nijuayo jinsi ya kufanya. Ndugu, cho chote ningalitenda kwa ajili ya mtu anayeketi pale katika hali hiyo, ningalitenda.

Na hebu niwaulize, mnaona. Wewe—wewe—wewe tayari umeponywa, kwa sababu Yesu alisema uliponywa. Mnaona, "Kwa mapigo Yake tuliponywa." Sasa kama ungeweza, kutoka ndani ya moyo wako, kukubali jambo hilo, hutakufa sasa, bali utaishi.

Sasa, unaona, sasa tunajua ya kwamba televisheni inakuja kupitia kwenye chumba hiki. Tunajua jambo hilo. Hatuioni. Hatuwezi kuliona, macho yetu hayajaumbwa, hisi zetu haziwezi kuichukua. Inahitaji bomba lililotengenezwa, au chochote kile, kioo, kuinasa.

Vivyo hivyo Mungu yupo. Hatumwoni, bali tunajua Yeye yupo hapa. Yesu Kristo ni yeye yule. Angalia, Yeye alijitangaza tu, jinsi anavyojifanya Mwenyewe. Sasa, kuhusu kuponya, kama Yeye alikuwa amesimama papa hapa sasa, asingeweza kukufanyia jambo lingine zaidi, mnaona, si jambo lingine. Kama Mwana wa Mungu alikuwa amesimama papa hapa, ambaye Yeye yupo, Yeye yupo hapa, bali asingeweza kukufanyia jambo lingine zaidi, kwa sababu tayari amejitambulisha Mwenyewe hapa. Mnaona? Naye yuko hapa sasa hivi, vivyo hivyo, kukuponya na kukufanya mzima.

78 Naye kijana mwanamke yule pale aliniambia, akisema, "Ulimwombea baraka, na kutabiri ama chochote kile juu yake, ya kwamba yeye angepata mtoto," akiketi kwenye kiti cha kusukumia wagonjwa. Naye akafanya hivyo, akampata mtoto wake.

Na sasa maskini mama huyu anayeketi hapa. Sasa yeye alikuwa na upasuaji wa tezi, na ulimfanya kupooza. Vema, tunaona mambo mengi sana yakitukia. Sasa, dada mdogo, ninajua wewe ni Mkristo halisi. Kwa nini Mungu amekuacha uketi pale, sijui. Ninaamini, labda, ni kwa sababu una … Imani, wewe—wewe unajaribu kupata imani, kutoka pale, waona; bali sasa tazama, tusijaribu tu kuwa nayo, na tuwe nayo sasa, waona, na ili tu—tuwe tunakwenda pale. Hilo tu ndilo jambo hilo, litaanza sasa hivi, nasi tutapata afya. Na ninyi watu huko nje katika viti hivyo, ninii, ama—ama chochote kile, kumbukeni tu ya kwamba Kristo yupo.

79 Sasa unasema, "Je! Kuna mtu fulani, unaona picha yangu ikipitia." Loo, naam.

Hata Maneno ya Yesu Kristo, aliyosema alipokuwa hapa duniani, yanapita moja kwa moja kwenye chumba hiki. Halifi kamwe. Ni wangapi wanaojua hiyo ni kweli kisayansi? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Vema, ni kitu gani? Ndipo Roho huchukua Neno hilo ambalo limeandikwa, na kulidhihirisha. Loo, utukufu!

Yeye yuko hapa. Yeye yuko papa hapa sasa, Bwana. Tunaninii tu … Tumeona mengi sana, Yeye amefanya mengi sana, mpaka kwa namna fulani tunajua, kwa namna fulani tunajikwaa. Laiti tungalitambua si kitu fulani cha kubuniwa, jambo la kitheolojia; bali ushahidi kwamba Yeye aliahidi angejidhihirisha mwenyewe katika majira haya, yupo hapa akiyaweka wazi haya mbele yetu sasa hivi. Ni jambo la ajabu iliyoje! Hilo si ni la ajabu? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.]

80 Sasa unaamini. Utaamini? Amini hautakufa. Utaishi, nawe utamheshimu Mungu. Utamheshimu Mungu. Umewahi kubatizwa? Wewe ni Mkristo, sivyo? Nawe ni Mkristo. Vema, unataka kuishi kwa ajili ya heshima ya Mungu. Basi nenda ukaishi, ndugu yangu. Katika Jina la Yesu Kristo, ishi!

Na, dada, unataka kutembea kwa ajili ya utukufu wa Mungu, na kumtunza mtoto wako mchanga; basi tembea, dada, katika Jina la Yesu Kristo!

Ninyi, kila mmoja wenu, fanyeni vivyo hivyo, katika Jina la Yesu Kristo! Msisahau hii Westward Ho Motel hapa usiku wa leo, Uwepo wa Mungu uliotambulika hapa. Yeye hana upendeleo. Yeye anataka tu uamini. Unamwamini sasa? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Amina. Mungu akubariki.

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa. Sijui wamemchagua nani, ku—kuturuhusu tutawanyike. Ndugu

Mushegian hapa, njoo papa hapa, ndugu. Yeye atataturuhusu tuondoke kwa maombi. Mungu akubariki.

MESSAGE hub online
www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7